Jumapili Novemba 26, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581506

www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 2

**70** wajitokeza kufanyiwa upasuaji maumbile ya mwili



UKURASA WA 3

**Othman** asisitiza viongozi kuweka mbele uzalendo




UKURASA WA 17

**Raia** wafurahia kuachiwa kwa mateka Israel



MAOMBI YANAMTOSHA VERA SIDIKA

UKURASA 20

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

# Onyo kwa watumiaji dawa nguvu za kiume

• **Madhara** yake ni baada ya miaka mitano, daktari atoa neno... *Ukurasa 2*





Matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume holela bila maelekezo kutoka kwa madaktari, mtu ataanza kuona athari zake baada ya miaka mitano na kuendelea, hasa kwa watu ambao huzitumia mara kwa mara, **Daktari Remigius Rugakingila.**

## Wakulima walia na baa la njaa athari za mvua

UKURASA 4



## Mama, mtoto wauawa kinyama, wahusika waondoka na vichwa

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA SC YABANWA NYUMBANI UK.24 KATUNI UK.6

# Watu 70 wajitokeza kufanyiwa upasuaji kurekebisha maumbile

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Idara ya Upasuaji Hospitali ya Taifa ya Muhimbili- Mlogazila, Dk. Erick Muhumba, amesema watu 70, wakiwamo wanaume, wamejitokeza katika awamu ya pili ya upasuaji rekebishi wa maumbile.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Dk. Muhumba alisema upasuaji huo unatarajiwa kufanyika hospitalini hapo Desemba 10, mwaka huu.

Dk. Muhumba alisema mwitikio wa watu ni mkubwa na wengi wao ni wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 45.

"Wengi waliojitokeza ni vijana na wanawake ambapo ni zaidi ya asilimia ya 70. Kwa siku tutafanya upasuaji kuanzia watu sita hadi 10 itategemea na aina ya upasuaji, kwa kuwa zipo zitakazofanyika kwa muda mfupi na nyingine muda mrefu," alisema.

Dk. Muhumba alisema upasuaji wa mafuta kupeleka sehemu nyingine, inaweza kutumia muda wa saa mbili.

"Bado hatujaanza kupokea malipo walioonyesha nia ni hao watu 70 kila upasuaji una gharama zake, kuna mwingine anataka kutoa kovu hii ina gharama yake, mwingine anataka kubadilisha matiti, mwingine anataka kurekebisha tumbo na mikono na mwingine kutoa mafuta gharama ni tofauti," alisema.

Dk. Muhumba alisema waliojitokeza wengi wao wanataka kuondoa mafuta tumboni na wengine wanataka kurekebisha mwonekano wa matiti yao kwa kuwa ni makubwa.

Pia alisema katika upasuaji huo, wapo wanaume waliojitokeza ambao wachache wanataka kutoa makovu na wengine kuondoa matiti.

Mtaalam huyo aliendelea kusisitiza kuwa, upasuaji wanaoufanya hakuna madhara kwa sababu wanazingatia uzito na urefu na afya ya mtu kuwa imara.



Wachuuzi wa mboga wakiwa wamepanga bidhaa zao wakisubiri wateja kwenye mazingira hatarishi kiafya kutokana na tope lililopo katika soko Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Onyo watumiaji dawa nguvu za kiume

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KASI ya matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume imekuwa ikiongezeka kila uchao kutokana na watu wengi kukumbwa na tatizo hilo. Sababu kubwa ni mfumo wa maisha hasa ulaji wa vyakula na matumizi ya vileo.

Kutokana na tatizo hilo, kumekuwa na matangazo mbalimbali yanayoshawishi watu kununua dawa hizo kwa kile kinachoitwa kurejesha heshima ya ndoa ndani ya nyumba.

Pamoja na kuwapo kwa kasi hiyo, watumiaji wa dawa hizo bila ushauri wa madaktari, kwa sababu ya watumiaji wengi kuingia kwenye maduka na kununua pamoja na wale wanaotumia miti shamba, wataalamu wameibuka na kuonya juu ya madhara yanayoweza kutokea.

Madaktari bingwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa, Dodoma, wameonya watumiaji holela wa dawa za kuongeza nguvu za kiume kuwa kufanya hivyo ni sawa na kutafuta furaha ya muda lakini baada ya muda wanaweza kupata madhara makubwa kiafya.

Kwa mujibu wa madaktari hao, athari za matumizi ya dawa hizo zinaweza kuonekana kuanzia miaka mitano tangu kuanza kutumia.

Katika mahojiano maalum na Nipashe, Daktari Bingwa wa Masuala ya Uzazi kwa Wanaume, Remigius Rugakingila, alisema kumekuwapo matumizi ya dawa hizo huku wengi wakinunua katika maduka ya dawa bila cheti cha daktari.

"Matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume holela bila maelekezo kutoka kwa madaktari, mtu ataanza kuona athari zake baada ya miaka mitano na kuendelea, hasa kwa watu ambao huzitumia mara kwa mara," alisema.

Dk. Rugakingila alibainisha kuwa tatizo la upungufu wa nguvu za kiume, liko kwa vijana na husababishwa na magonjwa ya akili, sukari, shinikizo la damu, ajali na msongo wa mawazo.

Alisema kutokana na matatizo hayo, jamii imekuwa ikitumia dawa hizo bila kupata maelekezo kutoka kwa daktari anayehusika na tatizo hilo. Alisema hana takwimu zinazoonyesha ukubwa wa tatizo hilo, lakini huwakumba vijana wengi na huchangiwa pia na kutojiamini wanapokuwa na wenza wao.

Kutojiamini huko, alisema husababisha kuwa na wasiwasi na kushindwa kufanya tendo la ndoa kwa mtu kujiona hana nguvu za kiume. Bingwa huyo alitahadharisha pia, wanaokwenda kwa waganga wa kienyeji badala ya hospitalini ili kupata matibabu sahihi na kutatua tatizo.

"Acheni kwenda kwa waganga, acheni pia kuona aibu kueleza matatizo ya nguvu za kiume kwa sababu wataalam wa kuwasaidia wapo,"alisisitiza Dk. Rugakingila.

**MADHARA**

Bingwa huyo alisema madhara kwa watumiaji yapo na kusisitiza kuwa hayatokei wakati mtumiaji ameanza kutumia dawa hizo, bali baada ya miaka mitano na mtu atashindwa kufanya kabisa.

Pia alisema matumizi ya dawa hizo huwafanya watu kushindwa kula vyakula stahiki ambavyo husaidia kuongeza nguvu za kiume.

"Ukiacha hilo si nguvu za kiume tu. Pia kuna tatizo la uzazi ambalo nalo huwafanya watu au vijana wawe na wasiwasi. Wataalam tunashauri mtu anapokwenda hospitalini aangaliwe vitu viwili, suala la uzazi na matatizo ya nguvu za kiume. Wakifanikiwa kutibiwa vyote hivyo, kila kitu kitakwenda sawa," alibainisha.

Kuhusu vijana, Dk. Rugakingila alisema kinachotakiwa kufanyika ni kuacha kuanza vitendo vya kujamiiana mapema kwa sababu kadri siku zinavyozidi kwenda huchoka na mwishowe huangukia katika matumizi dawa hizo.

**WATAALAM WA LISHE**

Mtaalam wa Lishe jijini Dodoma, Semeni Juma, alisema sababu kubwa inayochangia vijana kutokuwa na nguvu za kiume ni pamoja na kutozingatia mtindo sahihi wa ulaji wa vyakula.

"Ukiacha hilo pia, wanatakiwa kuzingatia mazoezi ili kuweka uwiano wa ulaji pamoja na kuweka afya vizuri ili kusaidia kuupa mwili nguvu," alisema mtaalam huyo.

Juma aliikumbusha jamii kuwa ni lazima mtu azingatie ulaji wa makundi matano ya vyakula ambayo ni vyakula vya asili ya nafaka, mizizi, ndizi mbichi, kundi la pili ni vyakula vya asili ya wanyama na jamii ya mikunde, kundi la tatu ni mboga, la nne ni matunda na la tano ni sukari, mafuta na asali.

Mtaalam huyo alisema wengi wamekuwa wakila chakula cha aina moja huku akionya kuwa ulaji wa chipsi peke yake hautoshi kuongeza nguvu na kujenga mwili.

"Hili tatizo si kwa wanaume peke yao, hata wanawake huwaletea shida katika uzazi pale wanaposhindwa kuzingatia makundi matano ya ulaji wa vyakula," alisema.

**VIJANA**

Kijana Jackson John mkazi jijini humo, alisema kwa sasa kuna tatizo kubwa la vijana kushindwa kufanya vizuri katika masuala ya ndoa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ulaji usiofaa.

"Unamkuta kijana amekaa baa badala ya kuagiza ugali wenye mboga na nyama za kutosha, anaagiza chipsi mayai. Hili ni tatizo kubwa," alisema.

Alisema ulaji usiofaa umechangia kwa kiasi kikubwa vijana wengi kujiingiza katika matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume ambazo zinauzwa katika maduka ya dawa na zingine kwa wanaouza dawa asilia.

Anthony Philemon, mkazi wa mkoani Dar es Salaam, alisema amekuwa akitumia dawa hizo kwa wiki mara moja ingawa hafahamu kama zina madhara hapo baadaye.

**DUKA LA DAWA**

Mfanyabiashara wa duka la dawa jijini Dodoma (jina limehifadhiwa) alikiri kuwa miongoni mwa dawa zinazonunuliwa ni pamoja na hizo za kuongeza nguvu mwilini.

Septemba 30, 2022, Rais Samia Suluhu Hassan, katika hafla ya utiaji saini Mkataba wa Usimamiaji wa Shughuli za Lishe, aliwataka Watanzania hasa vijana kula mlo kamili ili kujiongezea nguvu na afya ya kuzalisha watoto na kuongeza jamii.

Rais Samia alisema kuna athari kubwa ya lishe duniani na utapiamlo, na ulaji mbovu ambao hauwasumbui watoto tu bali mpaka wanaume ambao wako kwenye umri wa kuongeza familia. Alisema wanapokosa mlo mzuri, wanashindwa kufanikisha jukumu hilo.

# Othman asisitiza viongozi kuzingatia uzalendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema suala la viongozi kuweka mbele uzalendo, kuipenda nchi, kuamini na kujitoa ni misingi muhimu wa kuijenga nchi.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati akifungua kongamano la siku mbili la kumbukizi ya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad, lililowashirikisha viongozi wa vyama vya siasa, serikali , mabalozi na asasi za kiraia kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Othman alisema uzalendo katika uongozi unapaswa pia ushinde maslahi binafsi na usimame katika maslahi ya umma, sambamba na kujengwa katika imani ya kuwa mtu hawezi kupata uongozi kwa sababu ya nasaba au nafasi ya mrengo anaohusiana nao bali utokane na imani ya raia anaowatumikia.

Makamu huyo alisema ni muhimu pia kiongozi kuwa na uadilifu , ukweli, maono, ubunifu, kuyasimia na kukubali ulazima wa mabadiliko na kwenda na wakati.

Alisema nchi mbalimbali duniani kama Dubai na Singapore zimefanikiwa kiuchumi na kimaendeleo kutokana na kiwango cha juu cha uzalendo wa viongozi katika kusimamia maono, uadilifu na amani.

Kuhusu siasa na utawala, Othman alisema Tanzania imepitia katika vipindi tofauti lakini pia wananchi na viongozi wanatakiwa kuamini kwamba mfumo wa siasa za vyama vingi ni ushindani na si uadui na pia wananchi kuondokana na siasa za uhafidhina.

Alisema katika kupata maendeleo ni lazima kuwapo mfumo wa siasa unaotoa fursa na kuhimili mabadiliko na wanachi kuwa na fursa bora za kujiendeleza kiuchumi na kuendelezwa zaidi wananchi wanyonge na masikini ili nao wafaidi fursa za kujiendeleza kiuchumi na kujenga taifa lenye mshikamano endelevu.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema maono ya Maalim Seif ni kuendelea kuwa na taifa linalozingatia misingi ya haki za binadamu, kujenga umoja na mshikamano ili wananchi wote waishi kwa usawa na haki.

Hemed aliwataka Wazanzibari kuendelea kutunza na kuyaenzi kwa dhati maono hayo na kwamba ni muhimu kwa wananchi wote kubadili mtazamo kwa kuweka maslahi ya taifa mbele sambamba na kuzingatia amani na utulivu nchini.

Alisema vizazi vinatengemea kurithishwa amani na utulivu sambamba na kuwepo mabadiliko ya kweli ya kiuchumi na kwamba kinyume na hayo wanaweza kuwasema viongozi waliotangulia kwamba. Malengo ya kimaendeleo yafikiwe na taifa liendelee kuwa salama na lenye uchumi imara.


Mwanasiasa mashuhuri kutoka Afrika Kusini, Mmusi Maimane, alisema siasa na uongozi wa Afrika bado zinakabiliwa na changamoto kadhaa hivyo ipo haja kushikamana kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Alisema siasa za Afrika hazielekezi kutengana kwa mujibu wa maumbile wala uwezo na ni muhimu kila mmoja kushirikiana kwa pamoja katika kujenga nchi.

Mjumbe wa Halmahauri Kuu ya Taifa (NEC) Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mohamed Aboud Mohamed, alisema Maalim anakumbukwa kwa sababu ya sifa zake njema na uongozi bora.

Alisema sifa yake ya kwanza kubwa alikuwa mwenye subira, mvumilivu na mwenye kusamehe, pia hakuwa mbinafsi alijali maslahi ya taifa na aliamini zaidi katika mazungumzo katika kuleta muafaka.

Kongamano hilo limelenga maudhui ya " Siasa, Uongozi na Utawala: Tumekosea Wapi na Tujisahihishe". Mada tano zitawasilishwa, kujadiliwa na wataalamu kutoka ndani na nje ya Tanzania.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko (kulia), akikabidhi tuzo ya mshindi wa jumla kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, ya kutambua mlipakodi bora, wakati wa hafla za walipa kodi bora wa mwaka 2023 zilizoandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mama, mtoto wauawa kinyama, mhusika aondoka na vichwa vyao

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKAZI wa Kijiji cha Mavimba, Kata ya Milola, Wilaya ya Ulanga, mkoani Morogoro Mwanaisha Matele (37) na mtoto wake, Baraka Maita (7), wameuawa kikatili kwa kutenganishwa vichwa na viwiliwili kisha muuaji kuondoka na vichwa vyao.

Mauaji hayo yanadaiwa kutekelezwa na mtu ambaye walimkaribisha nyumbani kwao wiki mbili zilizopita.

Akizungumza na mwandishi wa gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mavimba, Salehe Ndopi, alisema tukio hilo lilitokea juzi saa 12:00 asubuhi katika Kitongoji cha Ilangali, Kijiji cha Mavimba na miili hiyo ilizikwa jana.

Ndopi alisema mtoto aliyeuawa ni mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Mavimba.

Alisema baada ya kupata taarifa kutoka kwa mwenyekiti wa kitongoji hicho asubuhi, alifika eneo la tukio na alipoingia ndani, alikuta miili ya watu hao na kutoa taarifa kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Tarafa ya Lupilo na Ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya Ulanga (OCD).

Uchunguzi wa awali, alisema ulionyesha miili hiyo imekatwa na vichwa vyote havikuonekana na kwamba mtuhumiwa wa mauaji hayo aliyatekeleza kwa kutumia kitu chenye ncha kali.

"Walifika hapa Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO), Mkuu wa Wilaya, mkurugenzi na uchunguzi ulifanyika na eneo la tukio kulionekana viwiliwili tu. Vichwa havikuonekana. Miili ilipelekwa Hospitali ya Mtakatifu Francis Ifakara kuhifadhiwa," alisema.

Alisema baadhi ya majirani na wapangaji wa nyumba hiyo walisema baba mwenye nyumba hiyo, alikuwa amesafiri kwenda mkoani Dodoma kwa ajili ya mahafali ya ndugu yake na alimwacha mgeni ambaye alifika nyumbani hapo wiki mbili zilizopita.

"Majirani walinieleza kuwa Novemba 24, mwaka huu, saa 11.00 alfajiri, huyo mgeni alionekana anaondoka akiwa na mabegi manne akienda sehemu ambayo haikufahamika," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema serikali ya kijiji imekuwa na utaratibu wa kuhakikisha mwananchi yeyote anayefikiwa na mgeni anatoa taarifa, lakini cha kushangaza familia hiyo haikutoa taarifa. Diwani wa Milola, wilayani Ulanga, Masudi Kilangongono, alisema tukio hilo limewaacha wananchi katika hali ya mshangao mkubwa.

"Tukio hili ni la kusikitisha na ni tatizo ambalo wananchi wamekuwa wakielezwa kuwa pale wanapofikiwa na mgeni wasiyemfahamu watoe taarifa kwa ajili ya utambulisho, wengi wao wamekuwa wakijisahau na badala yake wamekuwa wakiishi kwa kuaminiana.

"Taarifa za majirani ni kwamba mume wa marehemu Mwanaisha aliyefahamika kwa jina la Juma Maita, alileta mgeni huyo wiki mbili zilizopita na mtu ambaye aliwahi kukaa naye anaitwa Alex na wanafahamiana. Anashikiliwa na polisi," alisema.

Alisema mtu huyo aliomba akae na mgeni huyo kwa siku chache na angekuja kumchukua ili akafanye kazi za shambani.

Alisema katika kipindi alichokaa katika nyumba hiyo mtuhumiwa alikuwa akishiriki shughuli za nyumbani na kuonekana kuwa ni mtu asiyekuwa na shida.

Mkazi wa kijiji hicho, Rehema Lipangalalaa, alisema Mwanaisha enzi za uhai wake alikuwa hana tatizo na majirani wenzake aliishi nao vizuri.

Shomari Hassani, mkazi wa Kata ya Milola, alisema tukio hilo ni la kwanza kutokea na limeacha simanzi kubwa kijijini hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo simu zake ziliita bila majibu.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAFARI SAID SHABAN**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 693 DUC** aina ya **ALPHARD.** Chassis namba **ANH100027567.** Engine namba **2AZ1086836.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/7891/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA MOROGORO KITUO CHA MJINI**

**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......125/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SAID HUSSEIN NJAILA WA TUNGI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA RAMADHANI SAID NJAILA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 12 Mwezi 112 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

**Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 11 mwaka 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## ATHARI ZA MVUA

# Wakulima walia baa la njaa

Na Waandishi Wetu



WAKATI kukiripotiwa athari za vifo, uharibifu wa mali na miundombinu kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, wananchi katika maeneo mbalimbali wamesema kuna uwezekano wa kutokea baa la njaa kwa sababu ya mazao kuathiriwa.

Mvua hizo zimekuwa zikinyesha kwa muda mrefu katika baadhi ya mikoa ikiwamo Kagera, Geita na Mwanza, Tanga na Manyara huku mikoa mingine ikipata mvua za wastani zisizo na madhara yoyote.

Katika mkoa wa Kagera, baadhi ya wakazi wa wilayani Missenyi, wakizungumza na Nipashe, walisema mvua hizo zimesababisha hasara kubwa kwa wakulima baada ya mazao yaliyokuwa yameanza kustawi, yote kusombwa na maji. Walisema hali hiyo inaashiria kuibuka kwa baa la njaa.

"Madhara makubwa ni upande wa mazao. Wako waliolima mashamba makubwa kwa ajili ya biashara. Yote yameingiliwa na maji. Lakini hata sisi tuliolima kwa ajili ya chakula, yameharibiwa.

"Tulikuwa tunategemea mvua hii ituokoe baada ya jua kali la msimu uliopita lakini kwa mvua hizi, tunaiona njaa mbeleni," alisema Veronica Melchior, mkazi wa Kijiji cha Kenyana wilayani Missenyi.

Katika kata za Rwamishenye, Kashai na Hamgembe, Manispaa ya Bukoba, mvua hizo zimesababisha kifo na takriban nyumba 105 kuharibiwa. Diwani wa Rwamishenye, Sued Kagasheki, alisema serikali na wadau wamefanya tathimini na kutoa misaada kwa waliokabiliwa na janga hilo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima, alisema licha ya mvua hizo kuharibu makazi ya wananchi, pia zimeharibu majengo ya taasisi za serikali pamoja na kanisa.

Alisema hatua za awali zilizofanywa ni kuwatafutia makazi ya muda wakati ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri ikifanya tathmini ya namna watakavyosaidia kurekebisha majengo hayo.

### USAFIRI WASITISHWA

Mkoani Geita, wakazi wa Mtaa wa Nyakagwe, Halmashauri ya Mji wa Geita, walisitisha shughuli za usafiri na usafirishaji kwa muda wa saa nne kutokana na mvua kubwa iliyonyesha kwa saa moja na maji kuziba daraja linalounganisha barabara inayotoka Nyankumbu kwenda Kamena.

Mmoja wa wananchi hao, Magesa Francis, alisema mbali na kukwamisha usafiri, maji hayo yamefurika kwenye mashamba ya watu yaliyoko karibu na daraja hilo, hivyo kuomba serikali kuboresha miundombinu ili kuruhusu maji kutiririka zinaponyesha mvua kubwa.

"Tumelazimika kusubiri mvua ipungue kwani hata pikipiki kupita ilikuwa vigumu. Abiria waliokuwa wakisafiri kwenda Kakola walisitishiwa safari yao kwani gari lililokuwa linatokea Mwanza kwenda huko, limeshindwa kuendelea na safari ikabidi kurudi Mwanza," alisema Rebeca Said.

### WANAFUNZI WABEBWA

Kutokana na athari za mvua hizo, wako wanafunzi waliokuwa wakitokea Iponyamakalii kurejea nyumbani walioshindwa kuvuka eneo hilo hali iliyowalazimu baadhi ya vijana kuwabeba ili kuwavusha darajani hapo.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Geita, Frederick Mande, alikiri kuwapo kwa hali hiyo na kutaja chanzo kuwa ni shughuli za kibinadamu zinazofanyika karibu ya miundombinu ya barabara.

"Takataka zimeziba kwenye lile daraja hali iliyosababishwa na wananchi kufanya shughuli za kibinadamu, tulikusudia maji yapite pale. Hata tulipokwenda kukagua, tulikuta takataka nyingi za magogo yaliyofanya maji yashindwe kupita katika njia yake halisi, hivyo kupita juu," alisema.

Mkoani Mwanza, mvua hizo bado hajisababisha madhara makubwa licha ya kuharibu miundombinu ya barabara katika eneo la Chakechake, unapofanyika ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR). Hali hiyo imesababbisha kuwapo kwa msongamano wa magari mara kwa mara.

Kaimu Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Mrakibu (SF) Kamila Labani, aliliambia gazeti hili kuwa wananchi wameendelea kuchukua tahadhari kutokana na elimu waliyoitoa kabla, hivyo kupunguza madhara ya mvua.

Athari kubwa iliyosababishwa na mvua, Labani alisema hivi karibuni katika maeneo ya Mabatini wilayani Nyamagana, mtoto alibebwa na maji na jeshi hilo liliopoa mwili wake Ziwa Victoria.

"Mara nyingi maeneo korofi kwa hapa Mwanza ni Mkuyuni Darajani, Mabatini Pamoja na Kirumba, lakini hatujapokea taarifa zozote. Hii ni kutokana na elimu pamoja na jitihada tunazozichukua wakati wa mvua ikiwa ni pamoja na kufunga barabara kuzuia watu kupita kwenye mikondo mikubwa ya maji," alisema SF Labani.

Katika mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Tabora na Mara, mvua zinanyesha kawaida zikiambatana na jua la mara kwa mara, hivyo kufanya hali kuendelea kuwa salama.

### MUME, MKE WANUSURIKA

Watu wawili, mume na mke wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, wamenusurika kifo baada ya kuangukiwa na ukuta wa uzio wa nyumba jirani kutokana na mvua kunyesha.

Tukio hilo limetokea juzi katika eneo la Mdote, Kitongoji cha Majengo, ambako wanaoishi wanandoa hao, Juma Omari na mke wake, ambao wamelazwa Hospitali ya Teule Wilaya ya Muheza, huku hali zao zikiendelea vizuri. Wakizungumza na Nipashe, walisema ukuta ulioanguka ni wa uzio wa nyumba ya jirani yao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Shembekeza, Kata ya Kisiwani wilayani humo, Thobias Matheo, alisema katika kijiji chake, kaya saba zimehama baada ya kuzingirwa na maji ya mafuriko, hivyo zaidi ya wakazi 30 hawana mahali pa kuishi na wamehifadhiwa katika nyumba za majirani. Hali hiyo pia imetokea katika kata ya Kisiwani ambako mvua hiyo imesababisha hasara kubwa na wananchi kukosa makazi.

### BALAA MANYARA

Jeshi la Polisi Mkoa wa Manyara limesema toka mvua kuanza kunyesha katika msimu huu, vifo vilivyoripotiwa mkoani humo ni vya watu wawili huku nyumba 43 zikiezuliwa mapaa kutokana na upepo mkali na zingine 25 kuanguka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, alisema nyumba 43 zilizoezuliwa paa ni kutoka wilaya ya Hanan'g, Tarafa ya Balangdalalu na vifo vilitokea wilayani Mbulu.

Pia alisema wachimbaji watano walikuwa kwenye mgodi wa kijiji cha Tsawa na waliangukiwa na kifusi. Watatu kati yao walifanikiwa kutoka na wawili walipoteza maisha.

Alisema katika Kijiji cha Msitu wa Tembo kilichoko wilayani Simanjiro, mvua hizo zimesababisha nyumba 25 kubomoka.

**IMEANDALIWA na Vitus Audax, (MWZ), Alphonce Kabilondo (GEITA), Restuta Damian (KAGERA), Steven William (MUHEZA) na Jaliwason Jasson (BABATI)**

HABARI KITAIFA




Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Iringa, Paul Walalaze (kulia), akikabidhi cheti cha kutambua mlipakodi bora kwa Washauri wa kodi wa kampuni ya masuala ya ushauri wa kodi ya Assad Association Auditor, Sajjad Jusab (katikati) na Ajeet Katakia, wakati wa hafla ya walipa kodi bora wa mwaka 2023 iliyoandaliwa na TRA, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wahudumu mabasi kusajiliwa rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema kuanzia sasa wahudumu watakaofanya kazi katika vyombo vya moto vya kibiashara vya ardhini ni ambao wamepata mafunzo na kusajiliwa rasmi na mamlaka hiyo.

Miongoni mwa sifa za wahudumu watakaotakiwa kusajiliwa baada ya kupata mafunzo ni wenye lugha na kauli nzuri kwa abiria na walio nadhifu kuanzia mavazi na kila kitu.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa mafunzo kwa wahudumu wa vyombo vya moto huku akisisitiza kuwa, lengo lake ni kuhakikisha abiria wanapata huduma bora.

Alisema katika kuendesha mafunzo kwa wahudumu hao, watashirikiana na Chuo cha Usafirishaji (NIT) pamoja na Chuo cha Biashara (CBE).

Suluo alisema miongoni mwa mambo yatakayofundishwa kwenye mafunzo hayo ni pamoja na namna ya kutoa huduma ya kwanza iwapo abiria akipata changamoto zinazohitaji msaada, usalama kwa abiria na mali zao na utunzaji wa mizigo.

"Uamuzi wa mamlaka kutoa mafunzo kwa wahudumu kabla ya kuwasajili unatokana na kukosekana kwa wahudumu waliopata mafunzo rasmi katika sekta ya usafiri ardhini.

"Pia kukosekana uelewa wa sheria na kanuni za huduma za usafiri unaosababisha kuwapo kwa malalamiko mengi kutoka kwa abiria kuhusu mienendo isiyofaa ya wahudumu hao wanapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yao," alisema Suluo. Alisema katika mafunzo hayo, mkazo utawekwa kwenye ufahamu wa sheria, taratibu, kanuni na kujali wateja.

Pia alsiema kanuni itakayosisitizwa ni ile inayohusu usajili wa wahudumu ili wajue majukumu yao na pale wasipoyatimiza, maana yake wanatenda kosa lenye kustahili adhabu.

Suluo alisema moja ya masharti ya kanuni za udhibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu za mwaka 2020, ni kila mhudumu anayefanya kazi kwenye chombo cha usafiri cha kibiashara hususani magari ya abiria, kuhakikisha kuwa ana kadi ya usajili iliyotolewa LATRA.

Alitaja baadhi ya faida za kuwa na wahudumu waliopatiwa mafunzo na kusajiliwa kuwa ni pamoja na wamiliki kupata wasimamizi mahiri na wenye weledi wa kazi waliyopewa.

Pia alisema kufanya kazi kwa weledi na kuwa makini zaidi, abiria kuvutiwa na huduma nzuri, kurasimisha kazi hiyo ya uhudumu na kuifanya iheshimike kama zilivyo kazi nyingine.

Alisema kwa gari ambazo zitatumia mhudumu ambaye hajasajiliwa zitapewa adhabu ikiwamo kutoa faini ya fedha taslimu.

# Temeke yapigwa jeki vifaa usafi

**Na Beatrice Shayo**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Choo Duniani ambayo hufanyika Novemba 19 kila mwaka, Shirika la WaterAid Tanzania limetoa msaada wa vifaa vya usafi katika vituo viwili vya afya katika wilaya ya Temeke.

Vituo vilivyopatiwa msaada kupitia kampeni ya "Choo Safi, Hadhi Yangu" ni vya Mkondogwa kilichoko Chamanzi na Goroka kata ya Tuangoma.

Vifaa vya usafi vilivyotolewa ni pamoja na mifagio, sabuni, vifaa vya kuhifadhia taka, mabuti, majaketi ang'avu na glavu ngumu.

Akizungumza wakati wa kutoa msaada huo, Mkuu wa Sera, Ushawishi na Uraghabishi kutoka WaterAid, Christina Mhando, alisema vyoo ni suala la msingi na wanaamini kuwa kila mahali huduma ya choo ni muhimu.

"Nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwani hivi karibuni takwimu za afya za mwaka 2022 zinaonyesha kuna ongezeko la vyoo bora kutoka asilimia 21 mwaka 2016 hadi 75 mwaka 2022. Hiyo ni hatua nzuri Tanzania imefikia.

"Sisi WaterAid tunaendelea kuomba serikali mbali na uhamasishaji. kuelekeza rasilimali kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kila kituo kiwe na vyoo bora," alisema Christina.

Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Temeke, Dk. Timothy Bende, aliishikuru WaterAid kwa msaada huo ambao umekwenda kwa vituo vya afya vipya.

"Tunawashukuru kwa kutoa sapoti kwenye vituo hivi viwili vipya ambavyo vimekamilika mwaka huu na vimeshaanza kutoa huduma. Tumeonelea ni jambo jema vituo hivi vichanga kuweza kupata vifaa hivi kwaajili ya kuboresha na kuimarisha masuala ya usafi," amesema Dk. Bende.

Naye Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mkondogwa, Dk. Amri Mkwinda, alishukuru kwa msaada huo na kutoa wito kwa mashirika mengine kuwa na moyo kama huu kwani bado wana mahitaji mengi.

# Ujenzi wa hospitali wilaya wapunguza wagonjwa kusafiri hadi kilomita 387

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HOSPITALI ya wilaya ya Malinyi iliyojengwa kwa gharama ya Sh bilioni 3.3 kwa fedha za serikali kuu na kuwekwa vifaa vya kisasa, imesaidia kuokoa maisha ya wagonjwa waliokuwa wanasafirishwa kilometa 387 hadi katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Morogoro.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Rehema Bwasi, alisema hayo juzi mjini hapa huku akibainisha kuwa hayo ni mafanikio yaliyopatikana kipindi cha serikali ya sasa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya afya.

Alisema wilaya ya Malinyi iko pembezoni mwa mkoa na ilikuwa haina hospitali, hivyo wananchi walikuwa wanatumia fedha nyingi kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa wenye matatizo makubwa ya kiafya hadi hospitali ya rufani ya mkoa.

"Kwa muda mrefu Malinyi haikuwa na hospitali ya wilaya lakini uwapo wa hospitali hii umepunguza adha ya wagonjwa kusafiri umbali mrefu kwenda kwenye hospitali ya rufani ya mkoa wa Morogoro" alisema Bwasi.

Kwa kutambua changamoto hiyo, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 3.3 ambazo zimetumika kujenga hospitali ya wilaya yenye majengo 13 yaliyokamilishwa na yameanza kufanya kazi. "Kwa kweli hospitali imesaidia kupunguza vifo vya wagonjwa na pia kujengwa kwa vituo vya afya na zahanati, kumesaidia kuleta huduma karibu na wananchi," alisema.

Mkurugenzi mtendaji huyo alisema halmashauri ilipokea pia Sh bilioni 1.6 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba, kutoa huduma zikiwamo X- Ray , Ultrasound , vifaa vya huduma za upasuaji , meno na macho.

Katika hatua nyingine, serikali imetoa zaidi ya Sh. milioni 900 ambazo zimetumika kwenye ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Wilaya ya Ulanga ( Mahenge) iliyoko mkoani Morogoro.

Hospitali hiyo ilijengwa tangu mwaka 1905 wakati wa utawala wa kikoloni wa Mjerumani, ambao uliweka ngome katika eneo hilo wakati wa vita vya Majimaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Saida Mahugu, alisema licha ya kutolewa fedha za kukarabati, hospitali hiyo kongwe pia imewekewa mashine ya X-Ray iliyonunuliwa na serikali baada ya kusikia kilio cha wananchi.

Mahugu aliishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuboresha huduma ya afya maeneo ya mjini na vijijini kwa kujengwa vituo vya afya na zahanati.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mauaji ya kikatili yaliyoibuka yavizindue vyombo vya usalama

**KATIKA** siku mbili mfululizo, kumeripotiwa mauaji ya kikatili yanayodaiwa kufanywa na watu wasiojulikana katika maeneo mbalimbali. Miongoni mwa vitendo hivyo, vimeripotiwa kutokea katika mikoa ya Rukwa na Morogoro.

Mkoani Rukwa, imeripotiwa kuwa bibi mwenye umri wa miaka 60 aliuawa kwa kukatwa mapanga na watu wasiojulikana mbele ya wajukuu zake aliokuwa akiishi nao sababu kubwa ikidaiwa kuwa alikuwa akijihusisha na ushirikina.

Tukio kama hilo pia, limeripotiwa kutokea Malinyi mkoani Morogoro, baada ya mama na mtoto wake ambaye ni mwanafunzi kuuawa kinyama kwa kutenganishwa vichwa na viwiliwili kisha mhusika kutoweka na vichwa vyao. Katika tukio hilo, imedaiwa kuwa baba mwenye nyumba alimkaribisha mtu aliyedai kuwa ni rafiki yake na kwamba baada ya kusafiri kwenda Dodoma kwa masuala ya kifamilia, ndipo mgeni huyo alipofanya kitendo hicho cha kukatisha uhai wa mama na mtoto.

Kutokana na tukio hilo, taarifa zimeeleza kuwa miili ya wanafamilia hao imezikwa bila kuwa na vichwa jambo ambalo ni nadra kutokea katika jamii ya Kitanzania. Kama iliwahi kutokea, basi ni muda mrefu na kwa Watanzania wengi ni jambo geni.

Matukio kama hayo yalikuwa yakisikika mara kwa mara miaka ya 2000 yakilenga vikongwe na wenye ualbino kwa madai ya kuwashuku wazee hao kuwa ni washirikina na wanawaua watoto wa wahusika. Kwa upande wa mauaji ya wenye ualbino, yalikuwa yakitendeka kwa fikra potofu kwamba watu wenye ngozi ya aina hiyo ni 'dili' kwamba mtu anaweza kujipatia utajiri. Matukio kama hayo, kwa kiasi kikubwa, yalikuwa yakitokea katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Sambamba na hayo, katika mkoa wa Mbeya wakati huo (sasa Mbeya na Songwe baada ya kugawanywa), kulijitokeza magenge ya watu waliokuwa wakichuna ngozi binadamu wenzao kwa imani ile ile kwamba ni sehemu ya kujipatia utajiri katika shughuli za kibiashara na uchimbaji madini.

Vitendo hivyo vilishughulikiwa ipasavyo na vyombo vya dola na hatimaye kuwa historia baada ya waliokuwa wakijihusisha navyo kufikishwa katika vyombo vya dola na kuhukumiwa vifungo. Pia katika baadhi ya maeneo, waliokuwa wakishukiwa kujihusisha na mauaji na uchunaji ngozi, walipoteza maisha baada ya wananchi kujichukulia sheria mkononi.


Kuibuka kwa vitendo hivyo kunalirejesha taifa miaka kadhaa iliyopita wakati vitendo hivyo vilipokuwa vimetamalaki. Hatua hiyo sasa inaifanya jamii katika sehemu mbalimbali kuishi kwa hofu na wasiwasi juu ya maisha yao.

Kwa ujumla, matukio hayo si tu yanavunja na kutweza utu wa mtu na kupoteza nguvu kazi na unyonge kwa familia zinazoguswa bali vinaiweka nchi katika taswira mbaya kwenye jumuiya ya kimataifa.

Pia si jambo la busara kwa binadamu kuuawa kinyama namna hiyo, hivyo ni wakati sasa wa vyombo vilivyopewa dhamana ya kusimamia ulinzi na usalama wa raia, kuchukua hatua ili kukomesha kabisa unyama huo.

Matukio hayo yaliyotokea Morogoro na Rukwa yaiamshe serikali kupitia vyombo vyake hususani Jeshi la Polisi, kwanza, kuwasaka na kuwatia nguvuni washukiwa wa vitendo hivyo. Pili, wananchi pia katika maeneo ya makazi yao, waimarishe ulinzi na usalama, ikiwamo kuwatimua na kuwaripoti watu wanaoingia katika sehemu zao ili kuwatambua makusudi ya ujio wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hujuma ujenzi sekondari wasichana kikwazo kwa elimu

**SHULE** 26 za sekondari kwa ajili ya wasichana za masomo ya sayansi na hisabati zinajengwa kila mkoa, kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo.

Hatua hiyo inatokana na kwamba, baadhi ya wanafunzi hasa wa kike, wamekuwa wakiyakimbia kwa maelezo kwamba ni magumu, ndipo serikali ikaamua kuja na mkakati huo.

Kutokana na mkakati huo, kwa sasa Sh. bilioni nne zinatumika kwa kila mkoa kujenga shule hizo mpya, ili kukabiliana na changamoto iliyopo ya masomo ya sanyansi kutopendwa na wasichana.

Lakini wakati serikali ikijitahidi kufanikisha mkakati huo, baadhi ya watu wameanza kufanya hujuma ambazo huenda zikasababisha lengo la serikali kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo kukwama.

Moja ya hujuma hizo ni mifuko zaidi 600 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 20, inayodaiwa kuwa ni ya ujenzi wa Shule ya sekondari ya wasichana ya mkoa wa Mara kukutwa katika nyumba ya mtu.

Shule hiyo inajengwa katika eneo la Bulamba, Halmashauri ya Wilaya Bunda, na kwamba mifuko hiyo ilikutwa nyumbani kwa mtu katika Kijiji cha Karukekere wilayani humo hivi karibuni.

Baada ya kushuhudia mifuko hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vincent Anney, anasema tukio hilo ni la aibu na halikubaliki, huku akithitibisha kuwa amejiridhisha kwamba saruji hiyo ni mali ya serikali.

Mkuu huyo anataja sababu ya kuthibitisha kuwa saruji hiyo ni mali ya serikali, kwa maelezo kuwa miradi ya serikali inajengwa kwa saruji yenye kiwango cha 42.5, tofauti na ile saruji ya mtaani ambayo ni 32.5.

Katika mazingira hayo ya hujuma, ni kweli miradi ya ujenzi wa sekondari hizo itakamilika kwa kiwango kinachotakiwa? Ninadhani ipo haja kwa serikali kufuatilia kwa karibu ujenzi wa sekondari hizo.

Inawezekana kukawa na hujuma ya aina hiyo au zaidi katika mikoa mingine inayotekeleza mradi wa ujenzi wa sekondari za mkoa kwa ajili ya masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa kike.

Septemba mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, alifanya ziara katika Wilaya ya Bunda na kushiriki uchimbaji wa kifusi na kukijaza kifusi katika baadhi ya majengo yanayoendelea kujengwa, kwa ajili ya sekondari ya wasichana ya mkoa wa Mara.

Moja ya maagizo yake yalikuwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri na Ofisi ya Katibu Tawala Msaidizi upande wa miundomboni, kufuatilia kwa ukaribu ujenzi wa sekondari hiyo ili ukamilike.

Kwa mujibu wa Mtanda, mikoa mingine shule hizo zimekamilika, anawataka kuongeza kasi ya ujenzi ili shule ikamilike haraka, lakini wakati anahimiza wapo wajanja wachache wanaofanya hujuma.

Saruji ya ujenzi wa sekondari hiyo kukutwa nyumbani kwa mtu badala ya sehemu maalum ya kuhifadhia vifaa vya ujenzi, ni wazi kwamba ujenzi ungeendelea kusuasua au kutekelezwa chini ya kiwango.

Kukamatwa mifuko ungekuwa mwanzo wa kufuatilia mikoa mingine kuona kama kuna hujuma za aina hiyo zinafanyika, vinginevyo inawezekana ujenzi wa sekondari hizo ukatelekezwa chini ya kiwango.

Huyo aliyekutwa na saruji nyumbani kwake anaweza kusaidia serikali kubaini wale wote wanaohujumu miradi ya umma na kuchukuliwa hatua za kisheria, ili kuwa fundisho kwa mhusika na wengine.

Kama ni mwananchi wa kawaida, ninadhani atawataja wale waliofikisha mifuko hiyo katika nyumba yake, ili iwe rahisi kuwabaini wale wanaohujumu miradi ya serikali inayotekelezwa Bunda.

Miaka ya nyuma hujuma zilikuwa ni sehemu ya kawaida katika ujenzi wa madarasa ya shule za msingi ambayo baadhi yake sakafu ilichakachuliwa, na wakati mwingine mbao za kapaulia nazo zilichakachuliwa.

Baadaye ni kama vitendo hivyo vilidhibitiwa, lakini kwa tukio la kukuta mifuko ya saruji inayotumika katika ujenzi wa sekondari ya wasichana mkoa wa Mara, ndani ya nyumba ya mtu, inawezekana vitendo hivyo bado vipo maeneo mengi. Ni vyema ufuatiliaji uwe wa hali ya juu.

# Kikwete afurahishwa ufanisi miradi TASAF

**Na Lusungu Helela,** IRINGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, ameupongeza uongozi wa mkoa wa Iringa kwa usimamizi mzuri katika utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Amesema kupitia usimamizi mzuri wa utelekezaji wa miradi hiyo, TASAF imetatua changamoto mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika kaya za walengwa pamoja na wananchi katika maeneo ya utekelezaji. Kikwete aliyasenma hayo juzi mjini hapa wakati akizungumza na walengwa wa TASAF wa Kata ya Ruaha iliyoko katika Manispaa ya Iringa baada ya kukagua daraja lililojengwa katika eneo la Kingemgosi ikiwa ni utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaotekelezwa na TASAF.

Taarifa ya TASAF mkoa wa Iringa, inaonyesha kuwa miradi 474 ikiwamo uchimbaji wa visima vya asili, utengenezaji wa barabara, uzibaji wa makorongo na kuanzishwa kwa mashamba ya korosho ilitekelezwa kati ya Julai, mwaka jana hadi Juni, mwaka huu.

Pia mkoa ulipokea jumla ya shilingi bilioni 10.3, kati ya hizo, Sh. bilioni 8.9 zilitolewa kwa walengwa 30,988 kutoka vijiji 585 wakati Sh. bilioni 21.6 zilikuwa kwa ajili ya usimamizi ngazi ya mkoa na halmashauri.

"Nimefarijika sana kwa namna shughuli za TASAF zinavofanyika hapa katika mkoa wa Iringa likiwamo daraja lililojengwa katika eneo la Kigenamgosi. Haya ni matokeo ya ushirikiano thabiti kati ya uongozi wa mkoa na watendaji wote wa TASAF," alisema.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Oscar Maduhu, aliwahakikishia walengwa wa TASAF kuwa waendelee kubuni miradi ya kimaendeleo kwa kuwa serikali imetanga Sh. Sh. bilioni 51 bilioni kwa ajili ya walengwa hao.

"TASAF inaendelea kuhakikisha walengwa wote wanahudumiwa ipasavyo ili kuwaondoa katika hali ya umaskini uliokithiri kupitia ruzuku, miradi ya ajira za muda na kuwapa elimu ya kuweka na kukopa katika vikundi mbalimbali," alisema Maduhu.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Veronika Kessy, amesema mpango wa TASAF umesaidia kuinua hali za uchumi kwa walengwa pamoja na kuchechemua biashara mbalimbali kwa wananchi wenye kipato cha chini.

Alisema utoaji fedha za mpango umewezesha kaya za walengwa kuboresha makazi na kujenga nyumba za matofali ya kuchoma na kuezeka kwa bati badala ya nyasi.

# Serikali yaanza maboresho vyuo vya ardhi

**Na Munir Shemweta,** MOROGORO

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeanza maboresho katika maeneo ya vyuo vyake vya Ardhi vya Morogoro (ARIMO) na Tabora (ARITA)

Hayo yalibainishwa juzi na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, wakati wa Mahafali ya 42 ya Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) yaliyofanyika chuoni hapa.

Alisema wizara imeanza kufanya mapitio ya sera ya wizara aliyoieleza kuwa ni ya siku nyingi na iliyojaa upungufu na kuweka wazi kuwa sera pendekezwa tayari imekamilika na kuwasilishwa kwa wadau pamoja na Baraza la Mawaziri.

"Hivi sasa sera pendekezwa imekwishakamilika na kuwasilishwa kwa wadau mbalimbali na tayari imekwishawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri, hivyo iko katika hatua nzuri. Ndani ya sera hiyo, vyuo vimepewa nafasi kubwa katika kuleta mageuzi makubwa ndani ya wizara," alisema.

Pinda alisema sera hiyo imetoa msukumo mpya wa vyuo vya kati vya Morogoro na Tabora pamoja na Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mafunzo ya Taarifa za Kijiografia kilichoanzishwa Dodoma na kuzinduliwa hivi karibuni na Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, kuwa na sheria itakayosimamia uendeshaji wa vyuo hivyo.

"Pamoja na kutambuliwa na mamlaka mbalimbali zinazosimamia mafunzo hapa nchini, bado vyuo vyetu vilikuwa havina sheria. Mfano Chuo cha Morogoro kilikuwa chini ya Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam ambapo sheria ya chuo hicho ilipotungwa ilikiondolea sifa chuo hiki kutumia sheria ile," alisema.

Naibu Waziri alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuijali wizara ya ardhi na kubainisha kuwa mabadiliko yote yanayoendelea katika wizara ameridhia kuendelea nayo sambamba na kukubali kuidhinisha miradi mikubwa ya kimkakati yenye fedha nyingi.

Mkuu wa ARIMO, Charles Saguda, alisema chuo kina changamoto kadhaa zinazoendelea kushughulikiwa na kubainisha kuwa baadhi zinahitaji msukumo wa wizara.

Ametoa mfano wa changamoto zinazohitaji msukumo wa wizara kuwa ni suala la vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi. Alisema mafunzo ya chuo hicho yanahitaji umahiri wa kutenda na siyo kusimulia hivyo ni muhimu kwa chuo kuwa na vifaa vya kutosha vya kujifunza umahiri huo wanaoenda kuufanya wanafunzi katika soko.

Aliitaja changamoto nyingine kuwa ni uchakavu wa miundombinu ya chuo inayoendelea kushughulikiea huku akisema chuo tayari kinao mpango kabambe na kwamba ana imani utakuwa mwaroabini wa changamoto hiyo.

## FIKRA MBADALA

# *Sheria ya Uchaguzi imerejesha mamlaka kwa wananchi*



**Pascal Mayalla**

LEO naendelea na uchambuzi wangu wa muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023, kwa muhtasari wa sura zote 10 za sheria hii, kuwaelimisha elimu ya uraia na elimu ya sheria na haki ili Watanzania tuitumie kikamilifu katika miezi mitatu iliyotolewa ya kutoa maoni na mapendekezo kwa lengo la kuboresha sheria hii.

Muswada huu unatunga Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023 ukiunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Hivi sasa masharti ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ni sheria moja na hutekelezwa na mamlaka moja ambayo ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Hapa ninapendekeza uchaguzi mkuu na ule wa serikali za mitaa, ufanyike siku moja na kusimamiwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Wiki iliyopita nilichambua sura ya kwanza mpaka ya tatu, lakini leo naendelea na sura zilizobaki ili kubainisha yaliyomo na nini mapendekezo yangu.

Sura ya Nne ya Muswada inaweka masharti yanayosimamia uchaguzi wa wabunge na imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu sifa za wagombea katika uchaguzi wa ubunge. Sehemu ya Pili inahusu uteuzi wa wagombea ubunge na inaainisha siku ya uteuzi, uteuzi wa wagombea, utaratibu wa namna ya kuweka dhamana kwa mgombea ubunge, masharti ya mgombea kuteuliwa kwa jimbo moja tu, pingamizi na uamuzi juu ya uhalali wa fomu ya uteuzi

Sura hii pia inaainisha utaratibu wa kufuatwa endapo kuna mgombea mmoja tu halali wa nafasi ya ubunge au endapo hakuna mgombea. Kwa mujibu wa sehemu hii, endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya ubunge ameteuliwa, mgombea huyo atapaswa kupigiwa kura na atatangazwa kuwa amechaguliwa endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa

Kwa maoni yangu, hili ni jambo jema, zuri na lenye maslahi kwa taifa kwa kurejesha mamlaka kwa wananchi. Sasa hakuna tena ushindi wa mtu kupita bila kupingwa. Kupita bila kupingwa kulifanya chama kuwachagulia wananchi kiongozi. Hii itaondoa zile figusu za kuzuia watu kugombea, kuwanunua wapinzani na kuzuia fomu kurejeshwa na mtu kutangazwa mshindi wa kupita bila kupingwa. Kwa sasa CCM ina wabunge 18 ambao wamepita bila kupingwa.

Sura ya Tano inahusu masharti ya uchaguzi wa madiwani na imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya Kwanza inabainisha masharti ya uendeshaji wa uchaguzi wa madiwani, muda wa kuwa madarakani, namna na wakati wa kuitisha uchaguzi mdogo na uwakilishi katika kata.

Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu sifa za mgombea na mazingira ya mtu kukosa sifa ya kuteuliwa katika uchaguzi huku Sehemu ya Tatu ikijumuisha masharti kuhusu siku ya uteuzi, uteuzi wa mgombea, dhamana za wagombea, utaratibu wa kuweka pingamizi na utaratibu unaopaswa kufuatwa ikiwa kuna mgombea mmoja tu wa nafasi ya udiwani au ikiwa hakuna mgombea.

Sura ya Sita inaweka masharti kuhusu uchaguzi, utaratibu wa kupiga kura na uteuzi wa wabunge na madiwani wanawake wa viti maalum. Sura hii imegawanyika katika sehemu sita huku Sehemu ya Kwanza ikiweka masharti mbalimbali kuhusu siku ya uchaguzi na tangazo la uchaguzi.

Kwa mujibu wa masharti hayo, taarifa ambazo zitakuwa katika tangazo la uchaguzi ni pamoja na siku na muda wa kuanza na kufunga upigaji kura, anwani ya vituo vya kupigia kura, wapigakura waliopangwa kwa kila kituo cha kupigia kura na taarifa za wagombea walioteuliwa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi. Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu mgombea kujitoa na utaratibu unaopaswa kufuatwa endapo mgombea atafariki au hakuna mgombea.

Sehemu ya Tatu inaweka masharti kuhusu kampeni za uchaguzi na namna kampeni zinavyopaswa kuendeshwa, ikiwa ni pamoja na masharti kuhusu kuwasilisha ratiba ya mikutano kwa msimamizi wa uchaguzi kwa lengo la kuepuka migongano ya mikutano. Sehemu hii inaweka pia masharti kuhusu upatikanaji na wajibu wa vyombo vya habari vya umma na matakwa ya kutokuwa naupendeleo na kuepuka ubaguzi kwa mgombea yeyote katika utoaji wa matangazo.

Kwa maoni yangu, hapa bado kuna tatizo. Mgombea mmoja ana ving'ora, ana timu ya waandishi wa habari, ana magari ya serikali na watendakazi wa serikali!. Nchi za wenzetu, Rais aliyeko madarakani anapogombea tena, anaondolewa haki zote za urais isipokuwa ulinzi na wale wagombea wengine wote wa urais wanapatiwa ulinzi na mambo ya msingi tya usafiri. Kama ni ving'ora, wote ni ving'ora na si utaratibu wetu wa mgombea mmoja mwenye dola ameshika mpini kugombea kisu cha makali kuwili na wagombea makapuku. Unategemea ushindani wa haki?

Sehemu ya Nne ya Sura hii inaainisha utaratibu wa uchaguzi unaojumuisha masharti kuhusu siku na muda wa kupiga kura, mawakala wa upigaji kura, masanduku ya kura, muundo wa karatasi za kura na katazo la kuweka wazi kura.

Sehemu ya Tano inaweka masharti kuhusu utaratibu wa kupiga na kuhesabu kura. Masharti hayo yanajumuisha watu wanaostahili kupiga kura, mazingira yanayoweza kumfanya mtu kupotezasifa za kupiga kura, utaratibu wa kupiga kura, watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura, mazingira yanayoweza kusababisha kuahirishwa kwa upigaji kura inapotokea vurugu, kufungwa kwa zoezi la upigaji kura na utaratibu wa kuhesabu kura.

Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, mawakala wa upigaji kura wanatambuliwa kuwa mawakala wa kuhesabu kura. Vilevile sehemu hii inaainisha wajibu wa msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura, utaratibu wa kujumuisha kura katika uchaguzi wa wabunge na madiwani na utaratibu wa kutangaza matokeo ya ubunge na udiwani.

Sehemu ya Sita ya Sura hii inaweka masharti kuhusu uteuzi wa wabunge na madiwani wanawake viti maalum na unatambua utaratibu ulioainishwa katika Katiba na Sheria za Serikali za Mitaa kuhusu wabunge na madiwani wanawake viti maalum.

**Itaendelea wiki ijayo.**

**Wasalaam**
**Paskali**
**+255 754 270403**

## Ndalichako ataka Uzingatiaji sheria ya wenye ulemavu

**Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imewataka waajiri kuzingatia kifungu cha sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya mwaka 2010 kinachomtaka kila mwajiri aliyeajiri kuanzia watu 20 kuhakikisha asilimia tatu ya waajiriwa wake ni watu wenye ulemavu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira, na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Fimbo Nyeupe kitaifa yaliyofanyika mkoani hapa.

Alisema serikali inachukua juhudi katika kuimarisha ustawi wa watu wenye ulemavu hususani upande wa elimu, afya, miundombinu, ajira pamoja na ushiriki kwenye nafasi mbalimbali katika jamii.

"Nawapongeza pia kwa kutambua juhudi za serikali katika kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu ikiwamo kwa kuendelea kuwaajiri watu wenye ulemavu wakiwamo wasioona," alisema Prof. Ndalichako.

Alisema serikali imekuwa kinara katika kuthamini watu wenye ulemavu sambamba na kuboresha miundombinu ya shule za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Mwaka jana mwezi Desemba, Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya sherehe za miaka 61 ya Uhuru Sh. milioni 960 kujenga mabweni katika shule nane zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum wakiwamo wasioona," alikumbusha.

Prof. Ndalichako alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 serikali imetoa Sh. bilioni tatu kwa ajili kujenga vyuo vipya katika mikoa ya Kigoma, Ruvuma na Songwe.

Pia alisema kwa kushirikiana na wadau zimetolewa takribani Sh. milioni 500 kujenga chuo kipya Kisesa mkoani Mwanza.

Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLD), Omari Mpondelwa, alisema watu wasioona ni wapo kama watu wengine na kutaka jamii isiwanyanyapae.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alitoa rai kwa wazazi wenye watoto wenye mahitaji maalum mkoani humo kuwapeleka shule.

"Tunapoandikisha darasa la kwanza waacheni watoto waje shule na kama kuna mtoto ana changamoto Ofisa Elimu yupo, mwambie mtoto wangu anachangamoto hii ili kuangalia namna ya umsaidia," alisisitiza.

Kaimu Katibu Mkuu Taifa kutoka Chama cha Watu Wasioona(TLD), Subira Shedangio, katika risala yao alisema chama hicho kilianzishwa kutokana na madhila wanayokutana nayo ya kunyanyaswa kubaguliwa.

Shedangio alisema wanakabiliwa na changamoto ya gharama za bima za afya kuwa kubwa kwa watu wasioona kwa sababu hawana kipato cha uhakika.

"Kwa sasa kuna mabadiliko ya utoaji wa bima za afya mfano, watoto waliopo shuleni kuwa na idadi maalum, ambapo watoto wasioona wanaosoma katika shule za bweni na vitengo ambao hawawezi kutimia idadi hiyo kukosa huduma,"alisema Shedangio.

## Chuo cha kodi kufanywa kituo umahiri EAC

**Na Joseph Mwendapole**

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC) iko katika mchakato wa kukitangaza Chuo cha Kodi Tanzania (ITA) kuwa kituo chake cha umahiri katika utoaji wa elimu ya kodi na forodha kwenye ukanda huo. Hayo yalisemwa jana Mikocheni jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande, wakati wa mahafali ya 16 ya chuo hicho, ambapo wahitimu 508 walitunukiwa vyeti.

Wahitimu hao walitunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya Cheti, Shahada na Shahada ya Uzamili katika kozi mbalimbali za kodi na forodha.

Alisema chuo hicho kwa miaka 16 tangu kuanzishwa kwake kimefanyakazi kubwa ya kutoa wataalamu wa kodi na forodha kiasi cha kuwavutia watu wa mataifa ya jirani kuja kujifunza.

"Taarifa zilizopo ni kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki imekichagua chuo cha kodi kuwa kituo chake cha umahiri katika mafunzo ya forodha na kodi na mchakato wa ukitangaza unaendelea, hivyo ninapongeza baraza la chuo na menejimenti yake kwa mafanikio haya," alisema.

Alisema mchakato huo unadhihirisha kwamba chuo hicho ni muhimu na kina wajibu wa kipekee katika kuhakikisha kinatoa wataalamu mahiri katika kodi na forodha ambao watasaidia serikali kukusanya mapato.

Chande alikitaka chuo hicho kuendelea kufanya utafiti ambao zitaondoa changamoto katika mfumo wa kodi na forodha nchini, hali ambayo itarahisisha ulipaji wa kodi kwa hiyari na kuziba mianya yote ya ukwepaji wa kodi.

"Kwa kuwa tumefikia kiwango kikubwa hadi Jumuiya ya Afrika Mashariki kukichagua kuwa chuo chake cha umahiri yaani Center of Excellence ninawaomba muendelee na umahiri na ikiwezekana SADC nao waamue kukifanya chuo hiki kuwa kituo chake cha umahiri," alisema.

"Na hili wala siyo ndoto kwa sababu ninamini kabisa linawezekana kwa umahiri wenu na uwezo wenu mliojaliwa siyo EAC na SADC tu, hata Afrika inaweza kukichagua chuo hiki kuwa kituo chake cha umahiri kwa sababu sifa hizo mnazo," alisitiza.

Naibu Waziri Chande alisema lazima wataalamu wa chuo hicho wafanye utafiti wa kutatua changamoto za ukwepaji wa kodi hasa kwenye biashara ambazo zimekuwa zikifanyika mtandaoni.

Alisema serikali inatambua kuwa ziko biashara zinafanyika kwa njia ya mtandao, lakini bado haujatengenezwa mfumo mzuri wa kulipa kodi wakati duniani wameshaweka mifumo inayowawezesha kukusanya kodi za aina hiyo.

Alisema utozaji wa kodi ni jambo linalowahusu watu wengi kuanzia watunga sera, watozaji kodi na walipa kodi, hivyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inawajibu wa kusaidia chuo hicho kupanua wigo wa kutoa mafunzo ili nchi ipate wataalamu mahiri na wazalendo.

Alisema TRA inawajibu wa kuelimisha umma ili watambue wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi sahihi kwa hiyari na kwa wakati na kuiagiza iwe inatoa kozi fupi kwa walipa kodi.


Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alisema wameweka masharti kwa mfanyakazi wa mamlaka hiyo anayetaka kupanda daraja kupitia mafunzo katika chuo hicho kuongeza ujuzi wake.

Alisema chuo hicho kimekuwa na manufaa makubwa kwa mamlaka hiyo kwani tangu kianze kutoa mafunzo ya kodi na forodha miaka 16 iliyopita, kimefanikiwa kuzalisha maelfu ya wahitimu ambao wamekuwa wakifanyakazi nzuri kwenye mamlaka.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Isaya Jairo, alisema ITA ni mhimili wa TRA katika kukidhi mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wake ambapo asilimia 70 ya wafanyakazi wa mamlaka hiyo wanapata mafunzo chuoni hapo.

Alisema chuo kimeendelea kubuni na kutoa kozi mbalimbali pamoja na kuboresha mitaala na mazingira ya kufundishia ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wadau wake ya sasa na ya baadaye.

Prof. Jairo alisema chuo hicho kina dhamira ya kuwa kituo cha umahiri cha kimataifa katika mafunzo, utafiti na ushauri elekezi katika nyanja za forodha na elimu ya kodi.




Mshindi wa pesa taslimu Sh. Milioni 10 kupitia kampeni ya Vodacom Tanzania Plc inayoendelea ya 'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha', Lulu Kadege (kulia), akipokea mfano wa hundi kutoka Masta Shangwe, katika viwanja vya Kisonge, Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Upasuaji macho kufanywa kwa matundu madogo

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa macho kutoka Korea Kusini, inatarajia kuweka kambi maalumu ya upasuaji wa macho kwa njia ya matundu madogo kwa wagonjwa wenye matatizo ya mtoto wa jicho.

Kambi hiyo ambayo inaratibiwa na MNH kwa kushirikiana na Taasisi ya Vision Care, itafanyika kwa siku saba kuanzia kesho ikiwa ni mwendelezo wa kupanua wigo wake wa kutoa huduma za upasuaji kwa njia ya matundu madogo.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho ambaye pia ni Mkuu wa Idara ya Macho MNH Upanga, Joachim Kilemile, alisema upasuaji huo ni tofauti na uliokuwa unatumika awali ambao mgonjwa alikuwa anapasuliwa sehemu kubwa ili kutoa mtoto wa jicho.

"Upasuji huu ni wa kisasa zaidi mgonjwa atapasuliwa sehemu ndogo tofauti na ilivyokuwa ikifanyika awali. Muhimbili ni hospitali pekee ambayo inatoa huduma hii," alisema. Kuhusu faida za upasuaji huo, Dk. Kilemile alisema una faida nyingi kwa kuwa mgonjwa hupona kwa muda mfupi na kuendelea na shughuli zake kama kawaida.

"Mgonjwa atahudumiwa na kuruhusiwa siku hiyo hiyo kurejea nyumbani, atapona kwa muda mfupi na kuweza kuendelea na ratiba zake za kila siku. Awali mgonjwa alikuwa akifanyiwa upasuaji inamchukua zaidi ya wiki moja kupona na kurudi katika hali yake," alifafanua.

Dk. Kilemile ametoa wito kwa wagonjwa wote wenye changamoto ya mtoto wa jicho kufika Muhimbili Upanga kwa ajili ya kupata matibabu hayo.

Alisema kwa maelezo zaidi na kuweka miadi mtu anaweza kuwasiliana kupitia namba za simu 0713209056 au 0758261493 au 0713091664.

NOVEMBA 26, 2023
Nipashe

# MAISHA
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*



Ukurasa 14

**Sweta la kufuma**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Namna ya kubadili mwonekano wa nyumba yako



Ukurasa 12

**HARUSI**




# Sura isiyozeeka

Ukurasa 13

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | | U | G | A | L | I |
| B | | | | J | | M |
| W | | H | A | A | | B |
| A | R | A | | B | A | I |
| B | | M | B | U | | S |
| W | | I | | | | H |
| A | S | A | L | I | | A |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


GOA, JAA, LIA, WAO, EMORO, SHIBA, JOGOO, ILALA, ANGALIA, KIKWETE

## AMSHA AKILI

JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 4 | 2 | 3 | |
| 1 | | 2 | 4 |
| | | | |

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI



## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Careen alikuwa nyumbani akimsaidia mama yake kuosha vyombo. Wakati akiendelea na kazi hiyo mara alimuona mdudu jongoo akitembea karibu yake.

Careen aliogopa sana, alimwita mama yake ili amsaidie kumuua.

**Careen:** Mama jongoo ananikaribia njoo umuue

**Mama:** Hapana mwanangu, chukua mti msogeze hadi kwenye vichaka aendelee na safari yake.

**Careen:** Mama nikimtupa na mti wake itakuwaje ? Mwalimu wetu alitufundisha kwamba usimtupe jongoo na mti wake.

**Mama:** Hapana mwanangu huo ni msemo tu unaomaanisha tuwe na kumbukumbu kule tulikotoka na sio vinginevyo.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Baba anaposingiziwa mtoto kumbe mjukuu!

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vya Maisha ndivyo Yalivyo.Tuko katika siku za mwishoni mwa mwaka 2023. Vituko navyo haviishi kwenye maisha yetu.***

Mnapendana kwa dhati lakini penzi likiingia doa, ndipo vituko vyote vinakuwa hadharani au siyo? Hebu sikia kituko hiki.

Yuko kijana aliyemwoa ampendaye wakaishi kwa miaka kadhaa huku wakiomba Mwenyezi Mungu awajalie mtoto. Hata hivyo, hilo halikufanikiwa ndipo mzozo ukazuka kila mmoja akimlaumu mwenzake kuwa ndiye tatizo.

Kwa kuwa walikuwa wamefunga ndoa, mzozo huo ulifikishwa hadi mahakamani ili kuachana. Lakini wawili hawa walikuwa tayari wana mali ambazo ni nyumba na magari. Kila mmoja akadai agawiwe nusu kwa nusu mali zile walizochuma pamoja.

Lakini mashuhuda wanasema mwanamume huyo alikuwa ameendekeza sana ushirikina, hivyo akaenda kwa waganga kumloga mkewe ili asahau mali zote.

Hivyo ndivyo ilivyotokea kwani mbali na mahakama kuamua kuhusu mgawanyo wa mali,

> **"Mama baada ya muda akarudi Dar kwa mumewe akiwa na mtoto huyo mchanga ambaye kiukweli ni mjukuu wake (mtoto wa bintiye) na si wake wa kumzaa.**

bibie tangu waachane na bwana huyo hakurudi nyuma kudai tena chochote.

Inasemekana bibie alienda kuolewa kwingine na maisha yake yanamwendea vyema. Kwa upande wa mwanamume ndipo utamu wa habari hii ulipo kwani aliamua kuoa mwanamke mwingine haraka.

Lakini mke huyu si wa rika lake bali mtu mzima ambaye anakaribia kuwa mama yake wa kumzaa. Si unajua tena tabia za mashuga mami (mama watu wazima) na mashuga dadi (baba watu wazima) kuoa dogodogo?

Wadadisi wa mambo wanasema mama huyu kabla ya kuolewa na bwana mdogo huyu, alikuwa ameolewa na kuzaa watoto wakubwa, miongoni wakilingana kiumri na kijana huyu ambaye sasa ndiye mumewe. Hii ilikuwa siri hakuijua bwana huyu.

Mama huyu mtu mzima baada ya kuolewa na kijana huyu, wakaishi kwa muda ndipo akamwambia mumewe kuwa ni mjamzito. Mama huyu alikuwa bonge, mnene ambaye ukiambiwa ni mjamzito mwenyewe utakubali tu. Kumbe ilikuwa uongo, hakuwa na mimba wala nini. Ilikuwa fumbo mfumbie mjinga mwerevu alifumbue. Au siyo msomaji wangu?

Miezi ilivyosonga mbele akamwambia mumewe kwamba anataka kwenda kwao mkoani akajifungulie huko ili apate huduma nzuri kwani pale walikuwa wakiishi wao wawili tu. Jamaa akaingia kingi akakubali na kumruhusu.

Kumbe alikuwa anakwenda kwao ambako yuko binti yake aliyekuwa mjamzito na tayari walishapanga na mama yake kuwa akijifungua tu atamchukua huyo mtoto ili aje amsingizie mumewe kuwa ndiye mtoto aliyezaliwa. Hilo likafanyika kwa ustadi mkubwa.

Mama baada ya muda akarudi Dar kwa mumewe akiwa na mtoto huyo mchanga ambaye kiukweli ni mjukuu wake (mtoto wa bintiye) na si wake wa kumzaa.

Kurudi mumewe akafurahi kuona mama kajifungua mtoto, akampenda sana wala hakujua hilo ni changa la macho. Mtoto huyu akakua hadi kuanza chekechea. Baba akimfurahia sana. Ilifikia hatua wawili hawa wakabariki ndoa kanisani.

Na mtoto huyu kiukweli mama yake mzazi ambaye ni binti wa shugamami huyu, alimzaa na bwana ambaye waliachana na kurudi kukaa na mamaye.

Ikafikia wakati mama akaugua. Akawa hoi bin taaban wala haongei. Mume akachanganyikiwa kazi hana na huku anauguza.

Akaamua auze sehemu ya eneo analoishi kupata hela za kujikimu. Ile ameita mnunuzi, binti akamjia juu kwamba hana mamlaka ya kuuza. Akapiga ukunga (kelele), jambo ambalo lilivuta watu wakidhani pengine mama yule amefariki dunia.

Kisha baba huyu akamtaka binti kuondoka kwani yeye siyo baba yake na mama yake wamefunga naye ndoa kihalali.

Baada ya binti huyo kuambiwa hivyo, alikuja juu na kumwambia hawezi kuuza kiwanja hicho wakati mama yake yuko ndani akiugua na yeye hawezi kuondoka hapo nyumbani kwa sababu ni kwa mama yake mzazi.

Yule baba akasisitiza ni lazima aondoke kwa sababu nyumba hiyo ni ya mtoto wake aliyezaa na mama yake huyo. Kauli hiyo ilizua mzozo na ndipo binti huyo alimtamkia bayana baba huyo kuwa mtoto yule ni wake na na si aliyezaa na mamake. Baba hakukubali.

Binti hadi sana bado anavinjari pale anapougulia mamake na baba bado anasaka mtu ili auze nyumba wanayoishi abadili mwelekeo wa maisha. Je, una maoni? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Busara sawa, hesabu gharama kabla ya ugomvi

KILA kukicha hivi sasa, ukipitia mitandao ya kijamii, televisheni au magazeti ya kila siku, habari kubwa ni migogoro ya mapenzi, ndoa na uhusiano.

Kesi nyingi zinazoripotiwa ni za kuua kwa kukusudia, kuchinja au kumpiga mwenza kisu na kupoteza uhai. Ukifuatilia visa vyote hivyo, utagundua chanzo ni wivu wa mapenzi, hasa kuchepuka.

Takwimu za mauaji ya kikatili zinatisha. Hatujapata mwarobaini wa kupunguza tatizo.

Elimu inayotolewa na mashirika ya kiraia na serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, bado haitoshi.

Sasa, moja ya hasara kubwa za kufarakana ni kukosa busara kwa muda na kunyang'anywa utu na uwezo wa kupima gharama za hasara, kabla ya kutenda jambo.

Hasira ya dakika tatu mpaka tano, zimeacha doa kwa watu wengi kwenye mahusiano, pengine kuliko masuala ya kiuchumi.

Usianzishe vita kabla ya kupima gharama, kwa vile hata wana diplomasia wengi duniani, wanaamini kwamba kufuata njia ya amani kuna faida zote.

Kufarakana huvuruga aina zote za mafanikio, maendeleo na kufunga milango yote ya baraka zako.

Kama ni ugomvi kwenye familia, mahusiano au kwenye jamii ama kwenye taasisi, jitenge nazo, tafuta busara. Wengi wanakosa kaliba hii, hata taratibu za kistaarabu za kuishi kwao hutikiswa.

Haya yanayojitokeza sasa kwa wenzetu wenye mahusiano au ndoa, kuuana na wengine kuua watoto ili kujificha nyuma ya kukosa matunzo na ugumu wa maisha, yatufunze sote kuhesabu gharama kabla ya kugombana, ama kuchukua uamuzi mgumu wa kufanya ukatili.

Hapana shaka kwamba, mambo mengi yanayobishaniwa juu ya mahusiano na ndoa, yana nafasi kubwa ya kutafsiriwa katika Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 (Law of Marriage Act, Cap. 29).

Sheria hiyo inaelekeza vyema juu ya kuzingatiwa kwa kanuni za mashauri ya ndoa (matrimonial proceedings rules), kanuni za mabaraza ya usuluhishi wa ndoa (the marriage conciliation boards-procedure, regulations) na kanuni za ndoa kuhusu kazi za manaibu wasajili wakuu wa ndoa na talaka.

Umeona mambo hayaendi, mmechokana na hamuwezi kuendelea kuishi pamoja, fuata taratibu, achaneni kisheria.

Biashara ya kupigana, kuchomana visu, kupigana risasi, havina nafasi katika maisha ya kistaarabu.

Ifike mahali mlioachana kwa sababu mnazozijua ninyi wenyewe, msalimiane vizuri kama vile hamjawahi kupishana kauli, kuvurugana na kutengana.

Katika muktadha wa kisheria, ndoa imetafsiriwa kama uhusiano wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke.

Kwa muktadha huo, naiona njia bora ya kusuluhisha migogoro nje ya vyombo vya kisheria, kama Polisi na Mahakama (ADR), ni mwarobaini mpya wa matatizo haya.

Hivyo, kusuluhisha migogoro ya wana ndoa ni muhimu zaidi

> **"Umeona mambo hayaendi, mmechokana na hamuwezi kuendelea kuishi pamoja, fuata taratibu, achaneni kisheria.**

ili lengo la ndoa litimie la wanandoa, kuwa na uhusiano wa hiari kwa muda wote wa maisha yao.

Watanzania wengi wangependa kuona ndoa zao zinakwepa mitego ya kutumbukia katika migogoro, kwa ustawi wa jamii, taifa na familia husika.

Talaka iwe ni hatua ya mwisho ya utatuzi wa migogoro, baada ya wanandoa kupata fursa ya usuluhishi.

Ni nani mwenye uwezo wa kudai talaka, kati ya mume au mke? Jibu ni kwamba mume au mke, anaweza kuomba talaka iwapo amefanyiwa mambo au jambo, ambalo ni kinyume na matakwa ya sheria ya ndoa.

Hakuna mshindi katika kufarakana. Mafarakano huzaa hasara. Liwe somo kwa kila mmoja wetu kujifunza kuhesabu hasara, kabla ya kugombana.

***• Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

***Simu ya mkononi: +255 767 535490***

# HARUSI



Ni siku ya furaha kwa Nelson Kaise na Happiness Malima baada ya Novemba 19, mwaka huu kufunga ndoa katika Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis Dar es Salaam. Tunawaombea kwa Mungu ndoa yao idumu.

# MITINDO









## Sweta la kufuma

NGUO za aina ya sweta la kufuma kwa mikono inapendwa kuvaliwa kipindi cha baridi kutokana na sifa yake ya kipekee ya kuhifadhi joto.

Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kasi katika tasnia ya mitindo, vazi hili limekua likitumika katika nyakati zote za mwaka.

Mavazi ya aina hii hutumiwa na watu wa jinsia zote kutokana na umaridadi wake kuwavutia watu wengi.

Hata hivyo kumekuwepo na msisimko zaidi pale wabunifu wa mitindo huamua kujihusisha kwa ukaribu na aina hii ya nguo ambazo hufumwa kwa nyuzi nzito kwa mikono na sindano maalumu.

Unaweza kuvaa seti inayofanana kwa rangi ya sweta na sketi, suruali au viatu.

Ni vizuri rangi ya sweta na mavazi mengine yakafanana kwa uhalisia ili upendeze zaidi.


Sweta la kufuma unaweza kuvaa na fulana ya ndani maarufu kama vesti na kuunganisha na suruali.

Ikiwa ungependa kujaribu zaidi, vaa fulana kubwa chini unganisha na buti ndefu.

Aidha, Sweta ya kufuma unaweza kuvaa na 'blazer' ambayo itakupa mwonekano wa kuvutia.

Unaweza pia kuvaa sweta ya kawaida na blazer, bado utaonekana maridadi bila shida.

UREMBO







# Sura isiyozeeka

BAADHI ya wanawake bado wanaamini matumizi ya vipodozi vyenye kemikali ni dawa ya kuondoa mikunjo ya ngozi usoni.

Inawezekana ukapata tiba, lakini madhara yake yanajitokeza baadae husababisha majuto.

Kutokana na tiba nyingi za ngozi kuwa na kemikali nyingi hatarishi, ndio maana unashauriwa kutumia vipodozi vya asili.

Kuna njia rahisi ambazo zina uwezo wa kutatua tatizo la mikunjo bila kuhaha kutafuta katika maduka ya vipodozi ili kukabiliana na tatizo hili.

Tumia vitu vya kawaida vinavyopatikana nyumbani kuondoa mikunjo na kuufanya uso wako uonekane kijana zaidi.

Mahitaji ni tango, yai moja likiwa la kienyeji litapendeza zaidi na limao.

Tengeneza juisi ya tango vijiko 2, andaa ute mweupe yai na maji ya limao kijiko kimoja.

**Maandalizi**

Changanya vitu hivyo kwenye chombo kimoja na hakikisha kwamba vitu vyote vimechanganyika sawasawa. Hifadhi mchanganyiko huo tayari kwa kuupaka kwenye uso.



**Jinsi ya kutumia**

Osha uso wako kwa majisafi na sabuni na hakikisha umeukausha vizuri mara baada ya kuusafisha.

Paka mchanganyiko wako ulioandaa kwenye uso wako na acha kwa dakika15 hadi 20 kabla ya kuosha uso wako.

Osha uso wako kwa kutumia maji ya vuguvugu utaona mabadiliko na uso wako utakuwa umeshakuwa sawa.

Unaweza kufanya hivi kwa wiki mara mbili au moja.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Pika maharage kwa muda mfupi

MAHARAGE ni mboga inayotumiwa na watu wengi. Mapenzi ya maharage yanatokana na ladha yake tamu na ni nafuu kwa watu wa kipato cha chini.

Licha ya kuwa na ladha nzuri, lakini kikwazo kikubwa ni muda wa kuiandaa mboga hii. Zamani maharage yalichemshwa kwa nusu siku, lakini leo tunatumia muda mfupi kupika.

Leo tutaelekezana namna ya kupika maharage kwa muda mfupi kuepuka gharama ya gesi na mkaa.

Kwa kawaida, iwe ni maharagee ya njano au mekundu (maharage kitenge kama wengi wanavyopenda kuyaita), kulingana na eneo mapishi yake yanahitaji saa moja hadi nne hutumia kuyapika.

**Kuyaivisha haraka**

Chukua maharage kiasi ambacho umepanga kupika na kisha yaoshe. Weka maji kwenye chombo kulingana na kiasi cha maharage na ukubwa wa chombo kisha loweka.

Funika mboga hiyo na uiweke sehemu salama na usubiri kwa saa sita. Unaweza pia kuyaloweka kwenye maji ya moto ili kupunguza muda wa kusubiri.

Inashauriwa kuwa na chombo kinachohifadhi joto mfano chupa ya chai na hata "hot pot".

Weka maji ya moto kwenye chombo hicho kisha maharage. Subiri kwa saa moja hadi tatu yatakuwa tayari.



Baada ya hapo, toa maharage yako tayari kwa kupika kwa muda mfupi sana na kuyaunga.

MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

# Tengeneza mti wa familia ukutani, sio kwenye simu

MATUMIZI ya teknolojia yamepunguza baadhi ya vitu vilivyokuwa vinaziunganisha familia kutokana na namna mtu anavyoweza kuhifadhi baadhi ya kumbukumbu muhimu.

Moja ya kitu ambacho kimepoteza umaarufu ni albamu za picha ambazo ilikuwa ni kawaida ukifika kwenye familia unapewa kujionea baadhi ya matukio.

Jambo hili ni kama limepitwa na wakati kwa kuwa hivi sasa picha nyingi zinahifadhiwa kwenye simu na majukwaa ya kidijitali hivyo mtu akitaka kujua maisha ya rafiki zake ni rahisi kuyajua ndani ya muda mfupi.

Hata hivyo, wataalamu wa saikolojia wanashauri kuwa mti wa familia ni jambo ambalo kamwe halitapitwa na wakati.

"Family tree si jambo la kubeza, ni muhimu sana katika nyumba kuwepo ubao wa kuonesha historia ya baba na mama kuanzia kwa mababu," anasema Bahati Boaz, mwanasheria na mshauri wa masuala ya familia.

Anasema teknolojia ina mambo mengi mazuri japokuwa isipotumiwa vizuri itaua baadhi tamaduni na desturi nzuri ndani ya familia.

"Kwa sababu ni vigumu sana mtu akakuomba simu yako kuangalia picha na hata ikitokea ukampa mtu simu, huwezi kuwa na amani kwamba anaangalia tu picha...katika dunia ya ustaarabu hili si jambo zuri," anasema.

Badala yake anashauri kuwepo sehemu ya kuweka picha za kumbukumbu ya familia ukutani zikiwamo za mababu, wazazi, watoto na wajukuu.

"Unaweza kutumia hata ukuta mzima ukatengeneza kama maonesho ya picha hivi au sehemu ndogo ukaweka picha chache kulingana na utakavyoona inafaa," anasema.

Anasema uwekaji huu wa picha huamsha hisia nzuri ndani ya nyumba kwani ni rahisi kwa wanafamilia kuona matukio yao mara kwa mara na kujikumbusha hali iliyowatokea siku za nyuma kama furaha, huzuni au utani.





# Namna ya kubadili mwonekano wa nyumba yako



BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano.

Na mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa. Si vibaya kufanya hivyo, lakini hata pale bajeti inapokuwa ndogo unaweza kufanya maboresho hayo.

Miongoni mwa vitu ambavyo unaweza kuvitumia kubadilisha mwonekano wa nyumba yako hata bila kutumia gharama kubwa na ikapendeza ni pamoja na namna ya kuchagua rangi ya ukuta.

Nyingine ni matumizi tofauti ya karatasi za ukutani na malighafi nyingine zilizotumika kutengenezea samani zako ambavyo vikitumiwa vizuri vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa muonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.



Kwa mfano kupaka rangi upya kabati la luninga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa, nako kunasaidia kubadilisha muonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu kidogo kidogo kama vile tai na fimbo za pazia, pazia zenyewe, zuria, mapambo ya ukutani na mengineyo.

Viko vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke.

Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.


Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati na ndiyo maana huenda vinakuchosha na kuiona nyumba yako mbaya, usiikatie tamaa kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake.

Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza kidogo kidogo vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako hiyo, hata kama huna kipato kikubwa inawezekana, si lazima uweke vyote kwa pamoja, lakini kadri unavyojaaliwa unabadilisha cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati wa sasa.

Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine. Hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi kifupi, zuria ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati huu.

# KATUNI


JUKWAANI
KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
NYIE NYIE YULE 'UARABUNI' HUYU KWA 'NKAPA' ACHA NCHEKE
KAMA NILIWEKA NADHILI SIHAMI MJINI, ACHA IKANIDHULU
UKATA
KIJIJINI
NAKUONGEZA "SIKU MBILI" UKIFELI NAITIA "SOKONI"
HIVI NILIVYO "KUFAULU" LABDA BWANA ARUDI!
ZE BENKI
MKOPAJI
"BONDI" NYUMBA
ACHA KUJI-BALAGUZA HAKUNA WA KUKUKOPA
KAMA NDIO GIA "UMEDUNDA" NIMETOKA KUKABWA HAPO KICHOCHORONI!
UNANIKOMALIA NIKURUDISHIE MIA NNE YAKO, KISA GARI IMEHARIBIKA!.. INGEPINDUKA JE?
INGEPINDUKA NINGEKUKWIDA KABLA HATUJA-OKOLEWA.
NISHACHOKA KUKAA BILA KAZI!
AZIMA MIGUU UONDOKE!
BAR
ZAMANI NILIKUWA NIKIPENDA SIHOFII GHARAMA, SHETANI ALIKUWA MKALI
TWENDE AKAKUTANE NA KODI YA NYUMBA ILIYOKWISHA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MTOTO ALIYELALA NA SHIBE UTAMJUA ASUBUHI...

## HABARI KIMATAIFA





Baadhi ya raia wa Israel waliokuwa wakishikiliwa mateka na Hamas walioachiwa huru juzi

# Raia wafurahia mateka kuachiwa huru, wasambaziwa chakula, maji, mafuta

**TEL AVIV,** ISRAEL

MAKUBALIANO ya kubadilishana mateka yamepokelewa kwa furaha na wananchi wa Israel na Palestina, baada ya kundi la Hamas kuwaachia huru watu 24 waliokuwa wakiwashikilia.

Hata hivyo Israel imewaachia wafungwa 39, wakiwamo wanawake na watoto na kukabidhiwa mamlaka ya Wapalestina.

Mabadilishano hayo ni awamu ya kwanza chini ya mpango wa usitishwaji mapigano kwa siku nne.

Wapiganaji wa Hamas waliwaachia mateka kutoka Ukanda wa Gaza Ijumaa jioni katika siku ya kwanza ya kusitishwa vita hivyo, na baadae Israel iliwakabidhi wafungwa hao ambao walikuwa katika jela tofauti nchini humo.

Mateka hao walihamishwa kutoka Gaza na kukabidhiwa maofisa wa Misri katika kituo cha mpaka wa Rafah, wakiandamana na wafanyakazi wanane wa Shirika la kimataifa la Msalaba Mwekundu kwenye msafara wa magari manne.

Nchi ya Qatar ambayo inahusika na usuluhishi na kusimamia mpango huo wa usitishwaji mapigano ilisema Waisrael 13 waliachiwa huru, baadhi wakiwa wenye uraia pacha.

Katika mji wa Beituna wa Ukingo wa Magharibi, mamia ya Wapalestina walimiminika nje ya majengo ya makazi yao wakisherehekea kwa kupiga honi na kufyatua fataki.

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, aliapa kuwarudisha nyumbani mateka wote wanaoshikiliwa Gaza.

Jeshi la Israel lilisema mateka hao walifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu ndani ya ardhi ya Israel kabla ya kupelekwa hospitali na kukutanishwa na familia zao.

Msemaji wa jeshi,Daniel Hagari alisema watu wote wako katika hali nzuri.

Rais wa Marekani, Joe Biden alisema kuachiwa huru kwa mateka wa kwanza chini ya mpango kati ya Israel na kundi la wanamgambo wa Hamas ni mwanzo mzuri na kunatoa mwanga wa nafasi ya kurefusha makubaliano hayo.

Akizungumza na waandishi habari, Rais Biden alisema wanatarajia mateka zaidi kuachiwa jana na wengine leo na siku inayofuata.

Aliongeza kwamba umefika wakati wa kuanzisha upya kazi ya kuunda suluhisho la mataifa mawili kwa ajili ya amani kati ya Israel na Wapalestina.

Katika hatua nyingine, Umoja wa Mataifa ulisema malori 137 yaliyobeba msaada wa kiutu yaliingia Ukanda wa Gaza juzi. Ofisi ya umoja huo inayoshughulikia misaada ya kibinadamu (OCHA) ilisema kuwa wakati wa usitishwaji iliongeza upelekaji wa misaada ndani ya Gaza.

Ilieleza kuwa siku hiyo lita 129,000 za mafuta na malori manne yaliyobeba gesi pia yaliingia Gaza.

Huo ndio msafara mkubwa wa misaada ya kiutu kuingia Gaza tangu Oktoba 7, vita hiyo ilipoanza.

Shirika hilo lilisema maelfu ya watu wanaoishi Ukanda wa Gaza walipewa chakula, maji, bidhaa za matibabu na vifaa vingine muhimu vya kibinadamu.

**DW**




Wafungwa wa Kipalestina walioachiwa huru wakiwa katika gari la shirika la msalaba mwekundu

# Rais Rajoelina ashinda uchaguzi

**ANTANANARIVO,** MADAGASCAR

TUME ya Uchaguzi nchini Madagascar, imemtangaza Andry Rajoelina, kuwa mshindi wa nafasi ya urais na kumuwezesha kuongoza nchi hiyo kwa muhula wa pili.

Rajoelina (49), amepata asilimia 58.95 ya kura katika duru ya kwanza ya uchaguzi uliofanyika Novemba 16, mwaka huu. Tume hiyo ilitangaza jana kwamba rais huyo ameshinda kwa mara nyingine katika uchaguzi ambao ulisusiwa na wagombea wote wa upinzani. Idadi ya waliojitokeza kupiga kura ilikuwa ndogo baada ya wagombea 10 kati ya 12 wa upinzani kususia uchaguzi huo wakilalamikia mwenendo mbaya na kufananisha na mapinduzi ya kitaasisi kwa faida ya mgombea aliye madarakani.

**DW**

# DRC yataka kikosi cha EAC kuondoka

**ARUSHA,** TANZANIA

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imeendelea kushikilia msimamo wake wa kukataa kikosi cha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuongezewa muda wa kulinda amani eneo la mashariki mwa nchi hiyo.

Vikosi vya wanajeshi kutoka nchi wanachama wa jumuiya hiyo watatakiwa kuondoka baada ya kumaliza muda wao Desemba 8, mwaka huu..

Katika mkutano wa viongozi wakuu wa nchi wanachama uliofanyika nchini Tanzania, lakini rais wa Rwanda Paul Kagame na Felix Thisekedi wa DRC hawakuhudhuria.

Wakuu hao wa EAC walijadiliana kuhusu hali ya mashariki mwa DRC, ikiwamo kuchukua hatua zaidi za kukomesha mapigano mkoani Kivu Kaskazini.

Nchi saba kutoka ndani ya jumuiya hiyo zilipeleka vikosi vyao mashariki mwa DRC Novemba 2022 baada ya kuibuka kwa kundi la waasi la M23.

Hali ya kikosi hicho cha pamoja nchini Congo imekuwa ikitiliwa shaka baada ya Rais Tshisekedi kukikosoa utendaji kazi wake, lakini EAC iliamua kukiacha kikosi hicho nchini humo kwa miezi mitatu zaidi.

# Papa Francis augua mafua

**VATICAN,** ROMA

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis ameahirisha mikutano yake yote iliyokuwa imepangwa kutokana na kuugua ugonjwa wa mafua.

Taarifa iliyotolewa jana na Vatican, inakuja ikiwa wiki moja imebaki kabla kufanya ziara katika nchi ya Falme za Kiarabu kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa kimataifa wa hali ya hewa.

Papa Francis alipanga kwenda Dubai Desemba 2 kuhudhuria mkutano wa COP28, ambao anatarajiwa kukemea kukosekana kwa hatua ya kupunguza kwa kiasi kikubwa utoaji wa gesi chafu.

Afya ya Papa Francis imekuwa ikidhoofika katika miezi ya hivi karibuni, na kumlazimu kutumia kiti cha magurudumu na kuibua uvumi kuwa atajiuzulu kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake Papa Benedict wa XVI.

**DW**

## MAKALA

# SI KILA FURSA NI FURSA



Na Magabilo Masambu

**Ukweli ni kwamba tunapaswa kujifunza maisha kwa wengine lakini ni mwiko kuiga maisha hayo. Kila mtu ana siri ya mafanikio yake na wengi wanapoeleza juu ya mafanikio yao, huwa hawasemi ukweli. Mara nyingi husema sehemu tu ya yale watu wanayoyaona juu yao. Mambo ya sirini hawayasemi maana asili ya binadamu ni mbinafsi, hivyo si mara zote anapenda ufanikiwe kama yeye bali anataka tuheshimiane mjini.**

NI kweli kwamba kila mtu anayahitaji maisha mazuri lakini tusiyatafute kwa fujo kwa hofu kwamba tumekwishachelewa na hasa vijana wenzangu. Wakati mwingine si kila fursa ni fursa ya kutumia, hivyo lazima tuwe na muda wa kutafakari kabla ya kuchukua hatua.

Vinginevyo tutasababisha matatizo makubwa katika jamii kwa kudhani kwamba kila ambaye hajafanikiwa hakutumia nafasi yake vizuri. Lazima tukumbuke kila jambo na wakati wake.

Katika kuzungumza mambo mbalimbali na baadhi ya watu wenye umri mkubwa kuhusu maisha, nimegundua kwamba watu wengi wanapozeeka huwa wanajilaumu kwa mambo ambayo hawakuyafanya katika maisha na hawajutii kwa mambo ambayo waliyafanya ama kwa makosa au kwa kupatia.

Utasikia anasema "ningekuwa kijana, ningefanya hivi na vile au ungekuwa wakati wangu ningefanya hili na lile."

Ni kweli kuna umuhimu wa kufanya kila jambo kwa wakati lakini swali je, ni wakati gani sahihi wa kufanya jambo lipi?

Kuna mambo katika maisha unaweza kuyafanya kwa wakati lakini matokeo ya mambo hayo yakachelewa kutokea.

Mfano, unaweza kuoa ili upate watoto mapema lakini ukapata watoto katika uzee wako.

Katika maandiko kuna hadithi ya Bi. Sarai na Ibrahimu, katika umri wa miaka 99 ya Abrahamu na 89 ya Sarai, ndipo walipopata mtoto, baada ya kupewa taarifa na malaika kwamba: "Mwaka ujao wakati kama huu mtapata mtoto." Sasa sjui tunaweza kusema alichelewa au ndio wakati wake ulifika.

Kutokuwa na ndoto yoyote ya kutimiza katika maisha, inaweza kuwa sababu mojawapo ya kuona umechelewa, hivyo hustahili kufanya jambo fulani katika umri fulani.

Lakini kama unadhani kwamba kabla hujaondoka katika dunia hii, unatakiwa uwe umekamilisha ndoto yako au kusudi halisi la kuwepo duniani, basi msamiati wa kuchelewa unaweza kuwa sehemu ya maisha yako.

Wako watu wengi wanaofanya kazi ambazo kwa hakika wameshagundua hazitawafikisha wanakokutaka.

Kinachowafanya waogope kubadili kazi hizo ni kuona kwamba wamekwishachelewa kubadili kazi hizo na hasa wengi ambao wameajiriwa katika maeneo mbalimbali na sasa wanajaribu kutumia kila nafasi wanayoiona mbele yao bila kujua kwamba zingine ni za kuacha zipite ili kujiepusha na mambo mengi.

Dhana ya kutumia kila nafasi iliyoko katika kupata mafanikio, imewasababishia watu wengi matatizo makubwa.

Wengine wamepoteza maisha kwa kufanya kazi haramu, kujidhalilisha, kuugua peresha, sukari na matatizo mengine ya kiafya hasa pale wanapowaona marafiki, ndugu na jamaa wa karibu wakiwa na mafanikio makubwa.

Hata wengine ndoa zimevunjika kwa kukosa subira kwa kudhani mahali walipo si sahihi.

Ukweli ni kwamba tunapaswa kujifunza maisha kwa wengine lakini ni mwiko kuiga maisha hayo. Kila mtu ana siri ya mafanikio yake na wengi wanapoeleza juu ya mafanikio yao, huwa hawasemi ukweli. Mara nyingi husema sehemu tu ya yale watu wanayoyaona juu yao.

Mambo ya sirini hawayasemi maana asili ya binadamu ni mbinafsi, hivyo si mara zote anapenda ufanikiwe kama yeye bali anataka tuheshimiane mjini.

Tunachopaswa kufahamu ni kwamba hakuna siku tutayawahi Maisha.

Ndiyo maana hata wale wanaodhani wameyawahi hakuna siku wamepumzika kuyatafuta. Tutapumzika tu pale tutakapokuwa tumekata pumzi.

Hata kama ungekuwa tajiri, profesa au kiongozi mwenye madaraka kiasi gani, harakati zote hizo zitakoma kwa kufanikiwa kimaisha bali kifo.

Ukweli ni kwamba hakuna binadamu aliyeko duniani kimakosa. Suala la msingi ni kutafuta kusudi la kuwapo (purpose) ili ulitimize kabla ya kuondoka.

Haijalishi una umri gani unaweza kufanya maajabu katika umri wowote na wakati wowote na historia yako ikaandikwa na pengine ukaacha msaada mkubwa sana kwa watakaobaki.

Maisha ya jirani yako yasikuumize, tafuta yako taratibu kila mmoja na fungu lake!

Ni muhimu kuzingatia kuwa kila fursa inayokuja mbele yako ni kuitafakari kwa kina kabla ya kuchukua hatua yoyote kwa sababu fursa na nafasi hizo zimewafanya baadhi ya watu kwenye jamii kuishi maisha ya taabu na majuto.

Wako ambao wanaingia kwenye madeni makubwa kwa kudhani tu kwamba ni fursa za kufanya maendeleo. Matokeo yake wanageuzwa watumwa wa madeni na shida za watu wengine.

Ni kweli kwamba tuna shida nyingi lakini katika kuzitatua, unahitajika utulivu na umakini wa hali ya juu sana.

**0689157789**

**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kachukua mke wa mtu, kamsingizia mwenzake



Na Adam Fungamwango

**Mume akaamini kabisa hilo kwa sababu huyo mtu ndiye anayemrudisha mke wake kila wikiendi akitoka dansini. Akawaza kuwa kumbe huwa wanamaliza kila kitu ndiyo anamrudisha.**

UKIUSIKILIZA kwa haraka haraka wimbo wa 'Hasira Hasara' wa Juwata Jazz Band unaweza usipate picha kamili. Lakini kama utatuliza kichwa utapata ujumbe mmoja ambao utakuacha hoi. Kuna watu wa ajabu sana dunia hii.

Hiki ni kisa cha ukweli kabisa kilichompata mtunzi wa wimbo huo, marehemu Issa Ramadhani, 'Baba Isaya.'

Kuna rafiki yake fulani alikuwa anachukua mke wa mtu ambaye ni jirani yao, lakini akasingiziwa yeye ikawa balaa mtaani.

Moja kwa moja nianze na kisa chenyewe. Ni kwamba dada huyo alikuwa ni shabiki sana wa bendi ya Juwata Jazz, kila wikiendi ilikuwa ni lazima aende Msondo, ingawa alikuwa haendi na mumewe. Nadhani hakuwa shabiki wa muziki na pia alimwachia uhuru mkewe, hakutaka kumbanabana.

Dansi linapoisha kwa sababu anaishi jirani na mwanamuziki huyo ambaye alikuwa anapiga 'rhythm' na wakajuana kama ni majirani, alikuwa akimpatia lifti kwenye basi la wanamuziki.

Baba Isaya alikuwa anahakikisha dada yule anashuka, anagonga mlango na kuingia ndani, anafunguliwa na mumewe ndiyo anaondoka.

Kwa hali hiyo wote walizoeana na hakukuwa na wasiwasi wowote. Kumbe nyuma ya pazia kuna jamaa mmoja jirani akamtongoza dada huyo na wakawa wapenzi bila yoyote kufahamu.

Cha ajabu ni kwamba yule yule jamaa ambaye alikuwa anatembea na yule dada mke wa mtu akampelekea maneno ya uongo 'mume mwenza' kuwa Issa Ramadhani anatembea na mkewe. Akaacha kujisema anayetembea naye akamsingizia mtu anayemleta nyumbani usiku akitoka dansini.

Mume akaamini kabisa hilo kwa sababu huyo mtu ndiye anayemrudisha mke wake kila wikiendi akitoka dansini. Akawaza kuwa kumbe huwa wanamaliza kila kitu ndiyo anamrudisha.

Ikawa mshikeshike mapanga mkononi, nusura mwanamuziki huyo auawe na mwenye mali. Tangu hapo biashara ya yule dada dansini ikafa na uhusiano wa kijirani ukaisha. Hata hivyo, Baba Isaya akawa anashangaa kulishwa 'haramu' wakati yeye hajafanya kitu chochote.

Waswahili siku zote wanasema 'za mwizi arobaini', baada ya kisa mkasa.

Mume akapata data zote kuwa yule jamaa aliyemletea habari kuwa mwanamuziki Baba Isaya anatembea na mkewe, kumbe ni yeye ndiye anafanya kitu hicho, tena kwa ushahidi na si kuambiwa.

Kibaya zaidi ni kwamba baada ya sakata lile amempa talaka mkewe, lakini kabla hata mwaka haujatimia, Dora aliyekuwa mkewe na jamaa mwizi anayeitwa Kadiri wanafunga ndoa.

Baba Isaya hana hili wala lile yupo nyumbani kwake, akasikia hodi, alipofungua yule yule aliyemtuhumu kutembea na mkewe, akashtuka. Lakini akapozwa na kuambiwa hajaja kwa shari, bali heri.

Ndipo mume alipomwomba msamaha Baba Isaya, akisema alidanganywa na aliyemdanganya ndiye alimfuma anatembea na mkewe kwa hiyo wasameheane na waishi kama zamani. Yakaishia hapo.

Kwa Baba Isaya hayakuishia hapo. Akachukua kalamu na karatasi akaandika mashairi kuhusiana na kisa hiki, akakipeleka kwa wanamuziki wenzake, ambapo kuanzia wapigaji akiwemo yeye mwenyewe, waimbaji Nico Zengekala, TX Moshi William, Shaibu Monduli na Joseph Lusungu wakikitendea haki kisa hiki ndicho chanzo cha wimbo wa 'Hasira Hasara.'

"Naikumbuka siku ile, ulipokuja asubuhi na mapema, ukifoka kwa ukali kwamba mimi ndiyo niliyevunja ndoa yako.

Namshukuru baba mwenye nyumba aliyelizuia panga lako, lisifike maungoni mwangu, masikini nafikiria, ulivyotaka kunipa kilema cha maisha. Na leo hii nimefurahi, umegundua mzuri na mbaya wako.

"Ukweli nilikuja kwa hasira sana bila ya kufahamu undani wa mambo yenyewe.

Kadiri (mchukua mke wa mtu) aliniambia nilipokuwa safarini ulionekana na mke wangu kwenye majumba ya starehe.

Kadiri aliniambia ulipokuwa safarini ulionekana na mke wangu kwenye madisco na masinema. Nimeamini mzuri wako ndiye mbaya wako, na leo hii ni harusi ya Kadiri na Dora."

Hivyo ndivyo visa na mikasa ya watu duniani. Ndiyo maana wakati mwingine unaambiwa ukisikia jambo lifanyie uchunguzi kabla ya kufanya uamuzi au kuchukua hatua kwa sababu unaweza ukawa unaharibu zaidi.

Fikiria, yule jamaa angefanikiwa kumpiga panga Baba Isaya, vyovyote vile, amuue au kumjeruhi angeenda jela.

Unakwenda gerezani halafu huko anakuja mtu kukwambia kuwa yule aliyekuambia habari hizo kakuongopea, yeye ndiye anakuchukulia mkeo, yule uliyempiga panga wala hahusiki kabisa, wamemsingizia tu, utajisikiaje?

Shika la kuambiwa, jadili la kughafirika, kaa chini na upembue yasemwayo kwani yote si ya kweli, mengine mauzauza.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

# Kafie Kwenu-21

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




JAMES akazama mfukoni, akatoa noti nne za shilingi 10,000 akamkabidhi Catty.

“Hizi ni za maandalizi ya chakula Jumapili, najua wewe ni mtaalam wa kupika, nipikie chakula kizuri kama ulichokuwa unanipikia kipindi kile nilipokuwa naumwa.” Wote waliangua kicheko na kugongeana mikono.

“Na wewe husahau tu!”

“Kwa mapishi yale. Wali samaki mbichi, bamia, nyanya chungu, sijui na nini, weee.” James alisababisha Catty kucheka hadi machozi yakamtoka. Baada ya kutulia, James akiwa ametulia, akamwambia Catty.

“Nikija Jumapili nakuahidi kwa yote uliyowahi kunifanyia, nitakuletea zawadi kubwa ambayo hutoweza kuisahau.”

“Waooo!!! Haki ya Mungu wala sitolala usingizi, naisubiri hiyo zawadi inafananaje.”

******************************

Catty aliporejea kumsindikiza James, ile kuingia chumbani tu, Carry akaangua kilio kikubwa cha kwikwi na hisia kana kwamba amefiwa.

Kwanza kilio kile kilimshtua sana ndugu yake. Alijua kuwa tukio la James kubadilika na kuwa vile kulimuuma sana kwani ni mwanamke pekee ambaye alionekana kumpenda.

Akajua wazi kuwa kama ingetokea angemkubalia, saa hizi dada yake naye angekuwa ameukata, lakini hakudhania kuwa angeweza kulia kwa kiasi kile hasa ikizingatiwa ni yeye mwenyewe ndiye alikuwa anamkataa tena kwa maneno ya karaha, dharau na maudhi.

“Dada samahani, nimekosa na nimekukosea. Leo tunamkosa James hivi hivi. Ningekubali si angekuwa mikononi mwangu. Angekuwa mikononi mwetu.

Kama akipata mwanamke mwingine unafikiri anaweza kukubali awe na ukaribu huu ambao anao kwetu?” Akalia na kuomboleza.

Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi, amezungumza kitu cha maana sana na ametumia akili kubwa.

Ni kweli kama angemkubalia, basi leo hii utajiri wa James aliourithi kwa baba yake mzee Kamagi ungewahusu, lakini sasa imekuwa bure tu.

“Pole dada, lakini kumbuka nilikwambia.

Nilikwambia tangu mapema, siku zote usimdharau usiyemjua ila dada yangu hukutaka kunielewa.

Angalia sasa. Angalia sasa dada. Umepoteza bahati, tumepoteza bahati kubwa.

Kila kitu kinaonyesha kuwa mtu huyu angekuwa wetu, angetuchukua na sisi twende tukaishi kwenye jumba la kifahari.”

Akasema Catty na kuzidi kumtia uchungu dada yake ambaye alizidi kulia kwa hisia na kumlalia mapajani.

Mdogo mtu sasa akawa na kazi ya kumbembeleza dada yake, lakini bado na yeye moyoni ilimuuma

“Angalau ungemkataa kistaarabu asingekwazika sana, angechukulia tu kuwa ni kweli asingeweza kukumudu kwa wakati ule, lakini angekubali kwa sasa kukuchukua kwa sababu ana pesa na anaweza kukutunza, lakini vile kijana wa watu ulivyokuwa unamfanya, unamtolea mineno yako ya shombo na karaha, unafikiri hata wewe ndiyo ungefanyiwa hiyo ungekubali?” Catty alizidi kuongea, wakati huo huo akimbembeleza dada yake aliyekuwa akizidisha sauti kwa kulia.

**“Unaweza kumshawishi James akawa na wewe. Niko radhi kabisa James akuchukue wewe ili asituponyoke. Mimi kwangu imeshindikana, lakini wewe kwa sababu ni rafiki yake na mengi umemfanyia na amekuwa akikubali, anaweza kukubali uwe mpenzi wake akuoe!”**

Wakati huo Carry alilia mpaka nguvu zikawa zimemuishia. Sauti imemkauka.

Akiwa bado amejilaza kwa mdogo wake akajikakamua na kutoa sauti iliyosikika kwa mbali kwa mikwaruzo.

“Sikiliza mdogo wangu nikwambie.

Nina wazo moja, sijui kama linaweza kufanikiwa. Mimi nimemshawishi James nimeshindwa. Ila wewe unaweza kufanikiwa!”

“Kivipi?” Catty akashtuka.

“Unaweza kumshawishi James akawa na wewe. Niko radhi kabisa James akuchukue wewe ili asituponyoke.

Mimi kwangu imeshindikana, lakini wewe kwa sababu ni rafiki yake na mengi umemfanyia na amekuwa akikubali, anaweza kukubali uwe mpenzi wake akuoe!”

Catty akashangaa kama maneno haya yanatoka kweli kichwani kwa dada na akili zake timamu au amechanganyikiwa kwa sababu ya jambo hilo.

“Yeye alikuwa anakuhitaji wewe! Hakuna hata siku moja James aliyowahi kuniambia nakupenda hata kwa bahati mbaya pamoja na kuwa ni rafiki yake sana.

Pia tayari ameshaniambia kuwa ana mtu ambaye anampenda. Nadhani hili halipo, japo lingefuta machozi yetu.”

**********************************

Ni siku isiyosahaulika kamwe. James alifika nyumbani kwa kina Catty kama alivyoahidi. Hakuwa na chochote au mtu yeyote zaidi ya gari alilokuwa akiendesha Land Cruiser Prado. Iliwashangaza wengi hasa wanaomfahamu.

Catty alimpokea mgeni wake kama kawaida. Siku hiyo Carry naye alijikaza na kutabasamu japo moyoni ana maumivu kama kaa la moto. Hakukaa ndani kama alivyofanya siku ile ambayo alikuja.

Kila kitu kilienda kama kilivyopangwa. Mapishi yalifanyika ya hali ya juu.

Ulikuwa ni wali na samaki mbichi aina ya jodari aliyeungwa kwa nazi, nyanya chungu na bamia.

Catty aligundua kuwa James hupenda sana chakula hicho kwani wakati ule aliokuwa anakuja kula kwake wakati anaumwa alikuwa habakishi chakula siku akipika hivyo.

Ni kama kila kitu kilikuwa kimekwisha. Hakuna yeyote kati ya James na Carry aliyekuwa na kinyongo na mwenzake. Wakaongea, wakataniana.

Kulikuwa na watu watatu tu waliokuwa kama wanasherehekea kitu hivi. Ni James, Carry na Catty.

Chakula kilipoisha vinywaji vilichukua mahala pake. Ilipotimu saa sita kasoro dakika 20 hivi, ni kama James alishtuka hivi.

Akaangalia saa yake ukutani, akamwambia mwenyeji wake kuwa saa ya kuondoka imefika.

“Carry, saa ya kuondoka imefika, nadhani sasa ni wakati wangu wa kuondoka.” Akamgeukia Catty.

“Bibie, nadhani huu ni muda sahihi na mimi kuondoka, kwa leo nadhani imetosha mpaka siku nyingine tena nitakapokuja. Ila kabla sijaondoka unakumbuka kuwa nilikuahidi zawadi.”

“Nakumbuka, ndiyo nilikuwa naisubiri hiyo.” Catty akadakia.

Cha ajabu ni kwamba James hakuja na mzigo wowote wakati anaingia ambao unaonyesha labda amekuja na zawadi.

Catty akakumbuka kuwa amekuja na gari, huenda zawadi hiyo ipo ndani ya gari.

Wataondoka wote ili akaichukue.

James hakwenda popote, badala yake akasimama. Akaingiza mkono wake mfukoni. Catty akajua kumbe zawadi yenyewe ni pesa.

Wakati anatoa mkono, ghafla walisikia kitu kinaanguka chini na kubimbirika kikitoa mlio mkali.

ITAENDELEA JUMAPILI



# MAOMBI YANAMTOSHA VERA SIDIKA

MREMBO kutoka nchini Kenya, Vera Sidika ameibua sintofahamu kwa mashabiki zake baada ya kuwataka kumuombea aweze kupata nafuu.

Katika chapisho la Instagram, Vera hakuweka wazi tatizo linalomsumbua licha ya kueleza kuwa hali yake sio nzuri na kuhitaji maombi kutoka kwa mashabiki wake.

"Sijiskii vizuri,nikumbukeni nyote katika maombi," ameandika.

Kama haitoshi, Vera ameeleza kwamba huenda akajiondoa mitandaoni kwa muda mpaka pale atakapo pata nafuu.

# Benita kunogesha mitindo Tanzania

MBUNIFU wa mitindo anayefanya vizuri nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Benita Kanjinga Tshimi, amewasifu Watanzania kuwa na mwamko wa kutumia mavazi yaliyotengenezwa na wabunifu wa ndani.

Akizungumza hivi karibuni, Benita amesema kiu yake ni kuona tasnia hiyo inakuwa maarufu Afrika Mashariki kwa kuwatumia kikamilifu wabunifu na mafundi wachanga.

Benita ameteuliwa kuwa jaji mkuu katika maonyesho makubwa ya mavazi ya 'Afa Fashion Night' yatakayofanyika Jumapili wiki hii katika ukumbi wa Golden Memory Classic Hall Dar es Salaam.

Amesema anaamini kwa kutumia wabunifu wachanga wataleta uamsho kama ilivyo kwa nchi kama China inayosifika kutengeneza mavazi.

"Ushonaji wa cherehani sio kwa wale waliofeli maisha,  ni kazi inayotakiwa kutambulika sababu inasaidia na kuinua watu. Sasa tupo kwenye kuitangaza sekta itoke nje ya Tanzania, DRC au Kenya kwa watu duniani kote kuvaa nguo zinazotoka kwenye mataifa haya,"Amesema.

Aidha, amewashukuru wabunifu wa Tanzania kwa kumuunga mkono katika kutekeleza wazo hilo na kufikia daraja la kimataifa.

"Tutahitaji mafundi nguo wa mtaani wenye vibanda kutengeneza nguo, Mama Samia ametusaidia kutangaza utalii hivyo natamani wanavyokuja wanunue bidhaa zetu zenye mitindo ya Tanzania," amesisitiza.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### PHILLPIS, EKITIKE SOKONI

KLABU ya Newcastle United inapania kumsajili kwa mkopo kiungo wa Manchester City na England, Kalvin Phillips, 27, na mshambuliaji wa Paris St-Germain, Hugo Ekitike (21), katika dirisha la Januari. ***(Times)***

#### HOWE AMTAKA GUIRASSY

NEWCSTALE United chini ya kocha, Eddie Howe, wameonyesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Stuttgart na Guinea, Serhou Guirassy, 27, na mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin (26). ***(Teamtalk)***

#### BRENTFORD: TONEY HAUZWI

KLABU ya Brentford haina mpango wa kumuuza mshambuliaji wa England, Ivan Toney, 27, katika dirisha la Januari licha ya Arsenal na Chelsea kumwania nyota huyo. ***(Mirror)***

#### ANUKIA MANCHESTER UNITED

KLABU ya Manchester United imemfanya mlinzi wa Everton na England chini ya umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite. kama shabaha yao kuu ya safu ya ulinzi hapo mwakani. ***(Teamtalk)***

#### ERIKSEN ATAJWA SAUDIA

KLABU za Ligi Kuu Saudia zinafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United na Denmark, Christian Eriksen, 31, kwa pauni milioni 17 ifikapo Januari. ***(Caught offside)***

#### GRAY AGOMBEWA ENGLAND

KLABU ya Leeds United inajadiliana na kiungo wa England, Archie Gray na wanatazamiwa kupinga ombi la kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 wakati wa uhamisho wa Januari huku Liverpool, Everton na Crystal Palace zikiwa miongoni mwa timu zinazomhitaji. ***(Football Insider)***

#### MADRID KUMBANA ANCELOTTI

REAL Madrid inatazamiwa kumpa Kocha, Carlos Ancelotti, 64, mkataba mpya kwa lengo la kumbakiza katika klabu hiyo huku Brazil ikionyesha nia ya kutaka kumwajiri. ***(90 min)***

#### KUMBAKISHA GUNDOGAN

KOCHA wa Barcelona, Xavi amepinga tetesi kuhusiana na kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, 33, ataondoka katika klabu hiyo kuelekea Saudi Arabia mapema mwakani. ***(Goal.com)***

#### OUEDRAOGO ANUKIA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imewatangulia Manchester United na Chelsea katika mbio za kumwania mchezaji wa Schalke, Assan Ouedraogo, 17. ***(Teamtalk)***

#### CAUTO KUTUA MILAN

KLABU ya AC Milan inafikiria kumnunua beki wa Manchester City na Brazil, Yan Couto mwenye umri wa miaka 21, ambaye yuko kwa mkopo Girona inayoshiriki Ligi Kuu ya Hispania. ***(Clciomercato)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANE AWEKA HISTORIA YAKE BAYERN MUNICH

**MUNICH,** Ujerumani

● ● ● Ni mwingereza wa kwanza kufunga mabao mengi mapema katika...

HARRY Kane wa Bayern Munich alifunga bao pekee katikati ya kipindi cha kwanza wakati wa ushindi wa 1-0 dhidi ya FC Cologne hapo juzi na kumfanya aendeleze rekodi yake ya kufunga mabao mengi katika Ligi Kuu Ujerumani ( Bundesliga), huku akiipandisha timu yake kileleni kwa muda.

**Nahodha huyo wa England ambaye alikuwa usajili ghali zaidi Bundesliga alipojiunga na Bayern Munich akitokea Tottenham Hotspur kwa euro milioni 100 msimu huu, sasa amefikisha rekodi ya mabao 18 katika mechi 12 za mwanzo za ligi hiyo.**

Mshambuliaji huyo pia ndiye mchezaji wa kwanza wa England kufunga mara 18 katika msimu mmoja kwenye ligi Bundesliga, akizipita rekodi za mabao 17 zilizowekwa na Jadon Sancho na Kevin Keegan.

Bavaria hao ambao hawajapoteza mchezo kwenye ligi hiyo wana pointi 32, moja mbele ya Bayer Leverkusen ambao walisafiri kwenda kucheza na Werder Bremen walipo katikati ya msimamo hapo jana.

Cologne, wakiwa na ushindi mmoja pekee kutoka kwa mechi zao 12, wameendelea kuburuza mkia.

"Ulikuwa mchezo mzuri sana kwetu leo (juzi). Baadhi ya watu wanaangalia matokeo na wanaweza kutarajia zaidi. Lakini ulikuwa mchezo mzuri kutoka kwa kila mtu," alisema Kane.

"Tungeweza kufunga mabao matatu katika kipindi cha kwanza pekee.

"Matokeo yalikuwa jambo muhimu zaidi. Wao (Cologne) walicheza mipira mirefu michache katika kipindi cha pili, lakini tuliilinda pia. Haikuonekana kuwa hatari, ambayo ni ishara nzuri."

Mabingwa hao wa Ujerumani waliwazidi kabisa wenyeji mwanzoni na wakapata nafasi nyingi za kufunga, lakini hawakuzitumia ipasavyo.

HABARI MICHEZO



# TEN HAG: SIJAGOMBANA NA VARANE

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amekanusha taarifa za kutofautiana na beki wake, Raphaël Varane.

Varane mweye umri wa miaka 30 ameanza mechi moja tu kati ya nane zilizopita za United na amekuwa akihusishwa kuondoka Old Trafford ifikapo Januari, mwakani.

Ten Hag ana rekodi ya kutoelewana na wachezaji waandamizi wakiwamo, Cristiano Ronaldo na Jadon Sancho, lakini Mholanzi huyo amesisitiza kutokuwapo kwa Varane kwenye timu kunatokana na ushindani mkubwa wa namba.

"Rapha Varane? Sijui unachozungumzia," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari juzi alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kutoelewana na mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa.

"Ni uvumi. Mchezaji muhimu sana, lakini kuna ushindani wa ndani na lazima iwe hivyo kwa klabu kubwa kama sisi."

"Kinachozungumzwa ni hisia tu, lakini ukweli ni yeye ni mmoja wa wachezaji wakubwa.

"Kilichopo ushindani umekuwa ni mkubwa ndani ya kikosi, hivyo suala la kugombea namba ni la kawaida na hakuna kingine kinachoweza kufanyika zaidi ya kujitoa kwa mchezaji mwenyewe."

# Guardiola afunguka City hawana makosa

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameweka wazi klabu hiyo haina hatia hadi sasa licha ya kutuhumiwa katika 115 kupitia masuala ya matumizi ya fedha.


Guardiola amesema anajua watu wengi wanataka wafungiwe kama ambavyo Klabu nyingine vinavyofungiwa kwa kuvunja ya sheria ya haki ya usawa wa matumizi ya fedha kwenye usajili ( FFP).

Klabu ya Everton ndiyo ya hivi karibuni zaidi kukukumbwa na rungu la sheria hiyo kwa kukatwa pointi 10, lakini Guardiola amesisitiza klabu yake haina hatia.

Kocha huyo amesema kesi yao na ya Everton ambao wamepokonywa alama 10 wiki iliyopita ni kesi mbili tofauti kabisa, lakini akiwataka watu kutulia kwa sababu hadi sasa hawana hatia na wanasubiri uamuzi wa kamati.

City walituhumiwa kwa tuhuma 115 zinazohusiana na uvunjaji wa taratibu za matumizi ya fedha tangu mwaka jana, hivo wengi walitarajia wapate adhabu lakini hadi sasa hawajaadhibiwa.

Guardiola amesema anajua fika kabisa wengi wanataka kuona wanaadhibiwa, lakini hawawezi kuadhibiwa mpaka mashtaka yakamilike jambo ambalo hadi sasa halijatokea.





# Afrika Kusini yajitoa wenyeji Kombe la Dunia

**JOHANESBURG,** Afrika Kusini

AFRIKA Kusini imeondoa ombi lao la kuandaa Kombe la Dunia la Wanawake mwaka 2027, Shirikisho la Soka la nchi hiyo (SAFA), limetangaza.

Taifa hilo lilikuwa miongoni mwa nchi nne zilizothibitishwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kuomba mashindano hayo, lakini nchi hiyo badala yake itazingatia kuwasilisha ombi la mashindano ya mwaka 2031.

"Tuliona ilikuwa bora kuwasilisha zabuni iliyoandaliwa vyema kwa Kombe la Dunia la Wanawake la FIFA la 2031 na kuhakikisha tunaweka mguu wetu mbele, badala ya kutoa uwasilishaji wa haraka," Mkurugenzi Mtendaji wa SAFA, Lydia Monyepao, alisema kwenye tovuti rasmi ya shirikisho hilo.

Wagombea waliobakia kwenye zabuni hiyo ni Ubelgiji, Ujerumani na Uholanzi wanaomba kuandaa pamoja, Brazil na Mexico na Marekani ambao pia wanaomba kuandaa kwa pamoja.

FIFA litaamua nani waandaji wa michuano hiyo ifikapo Mei 17, mwakani. Australia na New Zealand waliandaa pamoja michuano ya mwaka huu 2023, ambapo Hispania ilishinda.

Marekani, Mexico na Canada zitaandaa Kombe la Wanaume kwa mwaka 2026.

HABARI MICHEZO

# Tanzania yatakata NBCA Golf Open

**Na Mwandishi Wetu**

MCHEZAJI wa kulipwa Mtanzania, Nuru Mollel, ameanza kwa kishindo katika mashindano ya wazi ya gofu (NBCA Tanzania Golf Open 2023) yanayoendelea kwenye viwanja vya Kili Golf jijini Arusha huku huku Kenya ikishika nafasi ya pili.

Mollel aliongoza kwa kupiga mikwaju 72 katika siku ya kwanza ya ufunguzi na mikwaju 74 katika siku ya pili, akifutiwa na Greg Snow wa Kenya aliyepiga mikwajua 77 na 73 kwenye michuano hiyo ya wazi inayodhaminiwa na Benki ya NCBA Tanzania kwa mara ya kwanza hapa nchini.

"Najisikia furaha kuongoza, michuano hii ni migumu, lakini nina amini wachezaji wa Tanzania tutafanya vizuri," alisema Mollel.

Kwa upande wa wachezaji wa ridhaa (wasiocheza michuano ya kulipwa), Godfrey Nsubuga (Divisheni A) kutoka Uganda ameendelea kuongoza kwa siku ya pili kwa kupiga mikwaju 72, akifuatiwa na Isiaka Daud wa Tanzania mwenye mikwaju 76.

Wachezaji kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Rwanda, Burundi, Ethiopia na Zambia wanashiriki michuano hii mshindi atajinyakulia Sh. milioni 10.

Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, ndiye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa michuano hiyo huku akiwa pia ni mmoja wa wachezaji mahiri wa mchezo huo.

Waziri Ndumbaro alielezea furaha yake ya kufanyika michezo hiyo na kuwakaribisha wachezaji wengine maarufu wa kigeni jijini Arusha, moja ya mikoa yenye vivutio vya utalii.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa NCBA Tanzania, Claver Serumaga, alisema benki ilikuwa na shauku ya kudhamini michuano hiyo kwa mara ya kwanza hapa nchini ili kushiriki kuuendeleza mchezo huo.

"Lengo kubwa ni kuona mchezo huu unakuwa mkubwa hapa Tanzania na kuwapa nafasi wachezaji kushindana na wachezaji wengine kutoka nchi za nje," alisema Serumaga.

Aliongeza benki hiyo pia inadhamini michuano ya gofu ya Afrika Mashariki hivyo imejikita kuhakikisha mchezo huo kuona unapiga hatua kubwa.

# KIPRE AFURAHIA KUFUNGA 'HAT-TRICK' LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Kipre Junior, ameonyesha furaha baada ya kufunga hat-trick wakati timu yake ikiichapa Mtibwa Sugar mabao 5-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi jioni.

Katika mechi hiyo ya raundi ya 10 ya Ligi Kuu, mchezaji huyo kutoka Ivory Coast alipachika mabao yake dakika ya 29, 43 na 63, ikiwa ni 'hat-trick' yake ya kwanza, lakini ikiwa ni ya nne mpaka sasa kwenye ligi hiyo msimu huu.

Mabao mengine katika mechi hiyo yalifungwa na Lusajo




Mwaikenda pamoja na Feisal Salum 'Fei Toto'.

"Najisikia vizuri, namshukuru Mungu kwa kufunga mabao matatu 'hat trick', kiwango cha timu kilikuwa kizuri, tunahitaji kuendelea mbele.

**Nimevutiwa zaidi na bao la kwanza lilikuwa bora sana, ulikuwa ni mjumuiko wa timu, yaani limetengenezwa na timu nzima, ni bao la pamoja, zuri na la kipekee, leo mimi kesho mwingine, nashukuru kila mmoja, tunasonga mbele," alisema Kipre.**

Rekodi zinaonyesha hiyo ni 'hat-trick' ya pili kwa Azam FC, ambapo ya kwanza ilifungwa na Fei Toto, lakini pia kati ya nne zilizopatikana mpaka sasa, tatu zimeihusisha timu hiyo.

'Hat-trick' ya Stephane Aziz Ki wa Yanga ilihusisha mechi ambayo Azam FC imecheza.

Ya kwanza ilikuwa Agosti 16, mwaka huu ilifungwa na Fei Toto kwenye uwanja huo huo, Azam ikiishindilia Tabora United mabao 4-0, kabla ya Jean Baleke wa Simba kufunga ya pili Septemba 21, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, akipachika mabao yote, Simba ikiichakaza Coastal Union magoli 3-0, na ya tatu ilipigwa Oktoba 13, mwaka huu na Aziz Ki, akiiongoza Yanga kuifumua Azam mabao 3-2, mchezo ukipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.




Mkurugenzi wa Tigo Zanzibar, Aziz Ali (kushoto) akimkabidhi zawadi ya fulana Mkuu wa Wilaya ya Mjini Zanzibar, Rashid Simai Msaraka (katikati) wakati wa uzinduzi wa shindano la 'Magifti Dabodabo' uliofanyika visiwani juzi. Kulia ni Meneja wa Tigo Kanda ya Unguja, Mwajuma Senkanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Shindano Magifti dabo dabo latikisa*

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHINDANO jipya kwa wateja wa huduma za Tigo la 'Magifti Dabo' limetikisa katika mikoa mbalimbali ikiwamo visiwani Zanzibar.

Shindano hilo lililozinduliwa jijini, Dar es Salaam hivi karibuni sasa limetambulishwa rasmi katika mikoa ya Arusha, Tanga, Mtwara, Mwanza na Zanzibar.

Mkurugenzi wa Tigo Zanzibar, Aziz Ali, alisema jana lengo la shindano hilo ni kuhakikisha wanatoa zawadi mbalimbali kwa wateja wao katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Alisema katika shindano hilo, washindi watajipatia zawadi mbalimbali zikiwamo fedha taslimu hadi Sh. milioni 30, safari za Zanzibar, Dubai na magari mawili mapya wakiwa na wapendwa wao.

"Tayari uzinduzi wa shindano la 'Magifti Dabo Dabo' umeshafanyika katika mikoa mbalimbali ikiwamo hapa Zanzibar, lengo ni kutoa zawadi katika kipindi cha mwisho wa mwaka kwa wateja wetu," alisema mkurugenzi huyo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mjini Zanzibar, Rashid Simai Msaraka, alisema shindano hilo linatarajiwa kuwanufaisha washindi kwa namna moja au nyingine.

Alisema wananchi watapata sehemu ya faida inayozalishwa na kampuni hiyo ikiwamo kupelekea mawasiliano vijijini, simu za mkopo na nyinginezo.

# Michezo

Jumapili Novemba 26, 2023

Nipashe




Ten Hag: Sijagombana na Varane UKURASA 22



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibanzokiza (mbele), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa ASEC Mimosas katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga yahamishia karata kwa Al Ahly

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa CR Belouizdad ya Algeria, Yanga imesema kwa sasa nguvu zote wanazielekeza katika mechi yao ya pili ya hatua ya makundi katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ukataochezwa Desemba Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salam.

Mabao ya Waarabu hao katika mechi hiyo ya Kundi D iliyochezwa juzi yaliwekwa wavuni na Abdelraouf Benguit, dakika ya 10, Abderrahme Meziane (dakika ya 45) na Lamin Jallow, sekunde chache kabla ya mechi hiyo kumalizika.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema hakuna haja au sababu yoyote ya kutafuta mchawi, au kufanya uchambuzi kwa nini wamefungwa na wapi waliemewa na badala yake wamekubali matokeo na sasa akili na nguvu zinaelekezwa katika mechi inayofuata.

Kamwe alisema matokeo hayo yameonekana kujirudia vile vile kama ilivyokuwa msimu uliopita katika michuano ya Kombe la Shirikisho walipofungwa na US Monastir ya Tunisia.

"Hakuna nafasi ya kufanya uchambuzi wa wapi tulielemewa, kilichotokea ni kitu ambacho huwa kinatokea kwenye mpira wa miguu mara zote. Yupo aliyetengeneza nafasi na akazitumia akaibuka na ushindi, yupo aliyemiliki mchezo, akatengeneza nafasi na akashindwa kuzitumia, ndiyo kilichotokea na mpira uko hivyo, ukianza kuchambua sijui imekuwaje unapoteza mwelekeo," alisema Kamwe.

# Simba yabanwa nyumbani

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### ●●● Yagawana pointi na ASEC Mimosas, Benchikha kuanza kibarua...

BAO lililofungwa na Pokou Serge dakika 12 kabla ya mechi kumalizika lilizima ndoto za Simba kuvuna pointi tatu kama kawaida yake inapocheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam baada ya kulazimishwa sare ya goli 1-1 dhidi ya ASEC Mimosas kutoka Ivory Coast.

**Serge aliunganisha mpira kutoka wingi ya kulia kwa Sankara Karamoto, aliyemhadaa beki wa Simba, Kenedy Juma na kupiga krosi ya nyuma ambayo iliunganishwa na mfungaji na kuwanyamazisha mashabiki wa Wekundu wa Msimbazi katika mechi hiyo ya kwanza ya Kundi B kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Simba ilikuwa ya kwanza kupata bao kwa penalti iliyowekwa wavuni na Saido Ntibanzokiza, dakika mbili kabla ya kwenda mapumziko, penalti hiyo ilitokana na beki ASEC Mimosas kuunawa mpira uliopigwa na Kibu Denis ndani ya eneo la hatari.

Muda mwingi wa kupindi cha pili, ASEC Mimosas walionekana kufunguka na kulitafuta goli kwa udi na uvumba na ilionekana wangepata wakati wowote kufuatia kupoteana kwa viungo pamoja na kukatika kwa mabeki wa Simba.

Pia wachezaji wa Simba akiwamo kipa, Ayoub Lakred, walionekana kuanza kupoteza muda, huku wakicheza kwa kuzuia zaidi badala ya kutafuta bao la pili.

Kosa la pili lilikuwa ni kupoteza mipira mingi kutokana na kushindwa kupiga hata pasi nne, badala yake mara kwa mara walipiga pasi mkaa, au kunyang'anywa.

Baada ya kupata bao, bado Asec Mimosas hawakuonekana kupaki basi, badala yake waliendelea kulisakama lango wa wenyeji wao ambao walionekana kushindwa kabisa kuipenya ngome ya wageni wao.

Kipindi cha kwanza, Simba ililisalimia lango la Asec dakika ya tatu ya mchezo kwa pasi mpenyezo ya Jean Baleke kwa Kibu, lakini akiwa eneo zuri tu kama angeweza kuumiliki mpira, lakini alishindwa kufanya hivyo ukatoka nje ikawa ni ahueni kwa wageni.

Kibu angeweza kuipatia Simba bao dakika ya 18, kama angeunganisha mpira wa krosi ya Israel Mwenda aliyeanza kwenye kikosi cha kwanza jana na kufanya vizuri sana, lakini aliukosa mpira huo, akipiga hewa na mpira ukapita chini ya mguu kabla ya kuokolewa na mabeki.

Dakika mbili baadaye, Kibu alikosa bao lingine aliposhindwa kulazimisha kuingia ndani ya eneo la hatari la Asec Mimosas kabla ya mabeki kumdhibiti na kuokoa hatari.

Mzamiri Yassin alikosa bao la wazi akiwa yeye na kipa, Ayayi ambaye alikuwa anamfuata, alichofanya kupiga mpira wa chini uliombabua kipa, badala ya kuupandisha juu kidogo.

Nafasi kubwa pekee ya kupata bao Simba ilipatikana dakika tano kabla ya mechi kumalizika, lakini shuti la Chama liliwababatiza mabeki wa Asec Mimosas, kabla ya Ayayi kuwahi kuudaka.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu mpya wa Simba, Abdelhak Benchikha, alitarajiwa kuwasili nchini jana tayari kuanza kibarua cha kukinoa kikosi hicho cha Wekundu wa Msimbazi akichukua mikoba iliyoachwa na Mbrazil Roberto Oliviera 'Robertinho'.

Benchikha ameingia makubaliano ya kuinoa Simba kwa muda wa mwaka mmoja na nusu anatarajiwa kuanza kazi rasmi baada ya mchezo wa jana dhidi ya ASEC Mimosas.

Akizungumza na gazeti hili, Benchikha alisema kila kitu kimekwenda sawa na anafurahi kuwa sehemu ya familia ya Simba huku akiahidi atahakikisha wanafikia malengo.

"Sasa nimekuwa kocha wa Simba na mapema nitawasili Tanzania kwa ajili ya kuanza kazi rasmi ya kuinoa timu hiyo ili kufikia malengo yanayotarajiwa na wanasimba. SIMBA NGUVU MOJA," alisema kocha huyo.

Msimu ulipota Benchikha aliipa USM Alger ya Algeria ubingwa wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kuifunga Yanga ya hapa nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >